# Nipashe

Jumamosi Desemba 5, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580420

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**TAMISEMI** yafunguka kuhusu 'mikopo umiza' kwa walimu wastaafu

UKURASA 3



**Kampuni** tano Austria zaonyesha nia ya kuwekeza Dodoma

UKURASA 9



**'Man United ipo pamoja na Solskjaer'**

UKURASA 22

# TAKUKURU: Mwarobaini rushwa ya ngono ni huu

UKURASA 2






Mabasi ya mikoani yakipakia abiria kando ya barabara ya Morogoro, nje ya kituo kipya cha mabasi ya mikoani na nchi jirani cha Mbezi Luis, jijini Dar es Salaam jana, licha ya Halmashauri ya Jiji kutangaza kuwa kituo hicho kingeanza kutoa huduma kuanzia Novemba 30, mwaka huu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Vinara tuhuma usafirishaji binadamu matatani

UKURASA 4

## Askari JWTZ mbaroni madai mauaji ya mkewe

UK. 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu



**MICHEZO** SIMBA 'TIK TAKA' KWA MKAPA LEO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Kikwete aipa somo UDSM ajira vijana

**Na Sabato Kasika**

RAIS Mstaafu, Dk. Jakaya Kikwete, amewataka wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kutilia mkazo katika elimu itakayowawezesha wahitimu kujiajiri na kuingia katika soko la ajira.

Alitoa rai hiyo jana chuoni hapo wakati akizindua programu mpya ya mafunzo ya kuwajengea uwezo zaidi wanafunzi ili waingie katika soko la ajira.

Dk. Kikwete alisema miaka 45 iliyopita, ajira zilikuwa zinasubiri watu, lakini leo hali imebadilika na watu wanahangaika kutafuta ajira, hivyo ni muhimu kuchukua hatua za kukabiliana na hali hiyo.

"UDSM jitahidini mtoe elimu na namna ya kutayarisha vijana ili hata kama watashindwa kuingia kwenye soko la ajira, basi waweze kujiajiri na kuendesha maisha yao," alisema.

Kikwete aliipongeza Empower Limited kwa namna ambayo imemua kushirikiana na UDSM katika kutoa elimu ya kuwezesha wanafunzi kuingia katika soko la ajira au kujiajiri.

"Ninawapongeza kwa kubuni wazo na kulifikisha hapa kwani mtu anaweza kuwa na mawazo mengi lakini yakaishia njiani. Hatua mlizochukua hadi kufikia hapa ni nzuri, wengine wajifunze kwenu," alisema.

Naye Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. William Anangisye, alisema wanafunzi wanakabiliwa na matatizo mengi ikiwamo la ukosefu wa ajira, wanapohitimu vyuo, kwamba wamejipanga kuyapunguza.

"Programu hii ambayo imezinduliwa, inakuja kujibu maswali magumu na hasa ya ukosefu wa ajira, kwani vijana watafundishwa mbinu mbalimbali zitakazowawezesha kuajiriwa ama kujiajiri," alisema Prof. Anangisye.

Mkurugenzi Mtendaji wa Empower Limited, Miranda Naiman, alisema programu hiyo ni ya karne ya 21 inayoitwa Generation Empower (GenEm) itakayoendeshwa na chuo hicho kwa kushirikiana na taasisi hiyo.

"Mafunzo yatatolewa katika shule zote za UDSM kwa kipindi cha miaka mitano ijayo na itahusisha wanafunzi 250 kila mwaka ambao wanatoka fani tofauti za taaluma na walengwa watapata ujuzi unaotakiwa," alisema Miranda.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa mafunzo hayo yataendeshwa kwa njia shirikishi na kwa vitendo zaidi, kwamba watashiriki semina za kubadilishana mawazo na pia mafunzo kutoka kwa wataalam.



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete akizungumza wakati akizindua programu mpya ya mafunzo ya kuwajengea uwezo zaidi wanafunzi ili wahimili soko la ajira, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TAKUKURU: Mwarobaini rushwa ya ngono huu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imetaja mwarobaini wa kumaliza rushwa ya ngono katika taasisi za elimu ya juu ikiwamo kuweka kiapo cha kutimiza kanuni za maadili kwa wahadhiri na walimu.

Ofisa utafiti wa TAKUKURU, John Juvinary, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utafiti walioufanya katika taasisi za elimu ya juu kuongezeka kwa vitendo hivyo.

Alisema kutokana na hali hiyo, mikakati mbalimbali imewekwa na TAKUKURU ili kukomesha rushwa ya ngono. Katika kutekeleza hilo, alisema kila taasisi ya elimu inatakiwa kuwa na kanuni za maadili zinazosisitiza misingi ya maadili ya kuharamisha rushwa.

"Kuwapo na kiapo cha kuapa cha wahadhiri na walimu kabla hawajaanza kufundisha kila mwanzoni mwa mwaka. Hii itasaidia sana kupunguza rushwa aina zote ikiwamo ya ngono," alisema.

Mbali na hatua hiyo, pia alitaja mkakati mwingine kuwa ni kuboresha mfumo wa usahihishaji wa mitihani ya wanafunzi, huku akitolea mfano kuwa mitihani isahihishwe kwenye jopo.

"Pia kuboreshwa kwa utoaji huduma za malazi ya wanavyuo kwa kuongeza matumizi ya kielektroniki ambayo itasaidia kupunguza kukutana na mtoa huduma," alisema Juvinary.

Kadhalika, alisema njia nyingine ya kukomesha vitendo hivyo ni kupitia Sheria ya TAKUKURU namba 11 ya mwaka 2007, ambayo inasema ili kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa ya ngono lazima uwapo uimarishaji wa dawati la jinsia na kamati za maadili katika taasisi za elimu ya juu.

Alisema mkakati mwingine ni kuwapatia wanafunzi miongozo ikiwamo kufundishwa sheria ndogo za chuo kuhusu wajibu wao na haki zao, kwamba kuwapo kwa kipengele cha rushwa ya ngono katika sheria ndogo za chuo, mfano kwenye sera ya jinsia.

"Mkakati mwingine ni kutoa maelekezo ya kusimamia muongozo wa kitaifa wa mavazi kwa watumishi wa umma, ili pia mkakati huo utumike katika taasisi za elimu ya juu nchini, ambayo itawakumbusha viongozi wa taasisi za elimu ya Juu kusimamia sheria, kanuni na taratibu katika usimamizi na utekelezaji wa masuala ya kitaaluma nchini," alisema Juvinary.

Ofisa huyo alisema mkakati mwingine ni kuwaondoa katika utumishi wa taasisi za elimu ya juu watumishi watakaobainika au kuhisiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa ya ngono, ikiwamo kuwachukulia hatua kali za kijinai.

"Lakini pia kuingiza elimu ya rushwa ya ngono kwenye mtaala wa elimu ili kuongeza uelewa kwa wanafunzi wa taasisi zote za elimu ya juu," alisema Juvinary.

Awali, akifungua kikao kazi hicho, Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa wa TAKUKURU, Sabina Seja, alizitaka taasisi kushirikiana na TAKUKURU katika kupambana na vitendo vya rushwa.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Chuo

Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Ombeni Msuya, alisema chuo hakipo tayari kuwavumilia watu wanaoendekeza kufanya vitendo vya rushwa ya aina yoyote.

Alisema wajibu wao ni kufanya kazi ya kutoa elimu kwa wanafunzi ili kuhakikisha wanapata wanafunzi walio bora.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Lulu Mahai, alisema wameanzisha dawati la jinsia kwa ajili ya wanafunzi kwenda kutoa taarifa zao juu ya unyanyasaji wa viashiria vya vitendo vya rushwa wanaofanyiwa na wahadhiri wakiwa chuoni hapo.

Alisema kila mwanafunzi anatoa taarifa kwa siri kupitia namba za simu ambazo wametoa kusaidia kufikisha taarifa hizo ili kumlinda mwanafunzi ambaye atatoa taarifa.

# Askari mbaroni tuhuma kumwua mkewe

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamshikilia askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Koplo Daniel Warioba (43), kutoka kikosi 92 KJ kwa tuhuma za kumuua mke wake, Joyce Ismail (35) ambaye ni mwalimu wa Shule ya Msingi Ruvu Darajani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tukio hilo limetokea usiku wa kuamkia jana huu katika eneo la Janga, Wilaya ya Kipolisi Mlandizi.

Kamanda Wankyo alisema askari huyo anadaiwa kumchoma mke wake na kitu chenye ncha kali sehemu mbalimbali za mwili na kumsababishia kifo.

Kwa mujibu wa Kamanda Wankyo, baada ya kutekeleza mauaji hayo, mtuhumiwa anadaiwa alitaka kunywa sumu kwa lengo la kujiua. Wankyo alisema polisi wamemkamata mtuhumiwa huyo na anaendelea kupata matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Tumbi, huku chanzo cha tukio hilo kikiendelea kuchunguzwa.

Katika tukio lingine, Kamanda Wankyo alisema Jeshi la Polisi linamsaka kijana ambaye anafahamika kwa jina maarufu la Bolizozo kwa tuhuma za kumuua Halima Said (50).

Kamanda Wankyo alisema tukio hilo lilitokea Desemba 2, mwaka huu, katika Kijiji cha Mpaji Wilaya ya Kipolisi Chalinze.

Alisema katika tukio hilo, inadaiwa Halima aliuawa kwa kukatwa na mapanga sehemu mbalimbali za mwili wake na kijana wake wa shamba ambaye jina lake halisi bado halijafahamika.

Alisema baada ya kufanya mauaji hayo, mtuhumiwa alikimbilia kusikojulikana, lakini Jeshi la Polisi bado linaendelea kumtafuta.

Wakati huo huo, Kamanda Wankyo alisema mwalimu wa Shule ya Sekondari Matipwili, Issa Mwakilasa (40), alichomewa nyumba anayoishi na kusababishiwa majeraha.

Kamanda Wankyo alisema tukio hilo lilitokea Novemba 30, mwaka huu, majira ya saa sita usiku, eneo la Matipwili huko Mkange na kwamba mwalimu huyo alijeruhiwa wakati akijiokoa kutoka katika nyumba hiyo.

Alisema thamani ya mali zilizoungua ni Sh. 235,000 na kwamba msako unaendelea kubaini watu waliohusika katika tukio hilo.

HABARI KITAIFA

# TAMISEMI yafunguka mikopo umiza ya walimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imewataka viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa semina ya athari zinazotokana na mikopo umiza kwa walimu, ili kujiepusha kukopa mikopo hiyo.

Aidha, imesema serikali imeanza utoaji mikopo yenye riba ndogo kwa watumishi, ikiwamo walimu kupitia halmashauri nchini ambayo zamani ilikuwa inatolewa kwa watumishi wa serikali kuu.

Wiki iliyopita Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Kahama, Mkoa wa Shinyanga, iliokoa na kurejesha Sh. milioni 23.6 za walimu wastaafu 19 waliokopa kutoka kwa wakopeshaji wa mikopo yenye riba kubwa.

Akizungumza jana na Nipashe, Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli, alisema ukopaji ni suala la hiari lakini walimu wanapaswa kupewa elimu kuhusu hasara ya mikopo hiyo ambayo inaonekana ina riba kubwa na inawaumiza.

Alisema viongozi hao wafanye semina za mara kwa mara ili walimu wapate elimu hiyo ya hasara na faida ya kukopa mikopo kwenye taasisi mbalimbali.

Mweli alisema kuwapo na programu maalum ya kuzungumza na walimu ili wawe na uelewa na imeanza kutoa mikopo kwa watumishi.

"Mimi nilienda ziara mkoani Tanga nikazungumza na walimu, nikawaambia kabla hawajakopa waangalie riba, kinachoumiza ni ile kuhamasishwa kuwa unapata ndani ya saa 24, anajikuta haangalii masharti mengine," alisema Mweli.

Hata hivyo, alisema serikali inapeleka kwenye Halmashauri kiasi cha kuanzia Sh.milioni 250 hadi 400 ili kusaidia kutoa mikopo kwa watumishi wa kada mbalimbali, wakiwamo walimu.

"Hii fedha ya mikopo kwa watumishi ni ile ambayo zamani ilikuwa inakuja serikali kuu, kuna halmashauri zimepelekewa hadi Sh.milioni 400 kwa ajili ya kukopesha watumishi, na ni njia ambayo serikali imechukua kuwaepusha na hiyo mikopo,"alisema Mweli.

Aidha, alisema masharti ya mkopo huo mtumishi hapaswi kuwa na mikopo mingine, lakini tatizo lililopo ni wengine kuwa na mikopo mingi, hali ambayo mkopo huo utamshinda kulipa.

Mweli alisema: "Kuna mwingine amefika kwenye theluthi moja ambayo hakopesheki, mimi naona elimu itolewe juu ya athari za kukopa fedha kwenye taasisi za kifedha, hatuwezi zuia wasikope ila wanatakiwa kuangalia masharti kabla ya kuumiza".




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisalimiana na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (NACOPHA), Leticia Mourice (kushoto), katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, kitaifa mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro mapema wiki hii. Katikati ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, Doroth Mwaluko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge kuibana serikali kuhusu wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema Bunge litahakikisha linaisimamia serikali kuwaondolea vikwazo watu wenye ulemavu katika upatikanaji wa mikopo ya halmashauri.

Amesema hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba mazingira yaliyopo hivi sasa si rafiki kwao na kuhimiza Sambamba na mikopo hiyo, amehimiza ujenzi wa miundombinu rafiki kwenye taasisi za serikali kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Spika Ndugai aliyasema hayo juzi wilayani Kongwa mkoani Dodoma wakati wa maadhimisho ya watu wenye ulemavu ambayo hufanyika Disemba 3, kila mwaka.

Ndugai alisema licha ya kuwa nao wanatambulika katika kupatiwa mikopo, watu wenye ulemavu wamekuwa na masharti magumu ikiwamo la kuwataka wajiunge katika vikundi vya watu watano.

"Neno vikundi linaleta matatizo makubwa na kupelekea (kusababisha) wengine kushindwa kupata mikopo kutokana na masharti yaliyowekwa," alisema Ndugai na kusisitiza kuwa mikopo inapaswa itolewe kwa ngazi ya familia na mtu mmoja mmoja kulingana na hitaji la mtu husika. "Haiwezekani watu wenye ulemavu kulazimishwa kuwa katika makundi wakati unakuta katika sehemu moja labda kuna wenye ulemavu wawili. Sasa kikundi kinataka watu watano, hao wengine wanapatikana wapi? Suala hili inabidi tulitazame upya," alisema.

"Nakubaliana nanyi kwamba masharti si rafiki, ila walengwa wanapochukua mikopo hii wahakikishe wanairudisha ili na wengine wapate fursa hiyo," aliongeza.

Awali, Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Tungi Mwanjala, aliomba serikali kutoa bure vifaa vya watu wenye ulemavu kutokana na vifaa hivyo kuuzwa bei ghali na hivyo wengi kushindwa kumudu gharama hizo.

Pia alitaja matatizo mengine ni pamoja na kutokuwa na miundombinu rafiki hasa katika majengo ya serikali, upatikanaji wa matibabu , ukosefu wa ofisi kwa wenye ulemavu, kutokuwepo kwa bajeti ya kutosha kwa watu wenye ulemavu na kuwapatia bima ya afya.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Selela, alisema maadhimisho ya mwaka huu yamelenga kuifikia jamii hasa ya vijijini kutokana na maadhimisho hayo kufanyika wilayani.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888, 40470
DODOMA
Tarehe 05/12/2020

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI** tarehe 05-12-2020 kampuni ya HAINAN INTERNATIONAL LTD itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SINGIDA** kuelekea **DAR ES SALAAM**, gari hilo lenye namba za usajili:

   T175DFN / T168DFN.

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 18.00 |
| Upana | - | mita | 2.82 |
| Kimo | - | mita | 5.00 |

3. Njia itakayotumika: **SINGIDA** hadi **DAR ES SALAAM** kupitia **MOROGORO**.

   Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

   Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MADAI NA. 65 YA 2020**

**APAISARIA ARNOLD KILWEO..........................MAREHEMU**
**Dhidi ya**
**ARNOLD BENARD SHIKONYI KILEWO..................MWOMBAJI**

Goodchance R. Lyimo, Advocate
Esq. Merik Law Attorneys,
P.O. Box 89006,
**DAR ES SALAAM.**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa aliyetajwa hapo juu, ameleta shauri la maombi ya madai dhidi yako; maombi ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi ya madai ambazo zinapatikana katika Mahakama hii. Hivyo basi, unahitajika kuhudhuria katika Mahakama hii kupitia Wakili au Mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe **22 DESEMBA, 2020 saa tatu (3:00)** kamili asubuhi mbele ya **Mhe. R.A. EBRAHIM, JUDGE,** kujibu maombi hayo dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia kwa ajili ya utetezi siku hiyo.

**ANGALIA:** Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.

**HATI** hii imetolewa kwa **AMRI** yangu na **CHAPA** ya Mahakama hii leo tarehe 04 Mwezi **DESEMBA, 2020.**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU – DAR ES SALAAM

## Polisi Kinondoni yatoa vifaa tiba

**Na Romana Mallya**

KATIKA kuhadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, Jeshi la Polisi Mkoa wa Kinondoni limetoa msaada wa vifaa mbalimbali katika Hospitali Kuu ya Jeshi hilo, Kilwa Road jijini Dar es Salaam.

Msaada huo ni pamoja na mashuka 30, viti maalum sita vya kubebea wagonjwa, mapazia maalum yanayotumika kuzungushia kitanda cha mgonjwa na vifaa vinavyohitajika kwa wagonjwa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, Kamishna Msaidizi (ACP) Ramadhani Kingai, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhi vifaa hivyo.

Mbali na msaada huo, jeshi hilo la polisi lilifanya usafi katika mazingira yanayozunguka hospitali hiyo na kutoa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Alisema Jeshi la Polisi litaendelea kuwakamata wale wote wanaojihusisha na vitendo hivyo kwa kuhakikisha wanafikishwa mahakamani ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya watakaokutwa na hatia.

"Mkiona kitendo cha kikatili kimefanyika tushirikiane kwa kumchukua aliyetenda kitendo hicho na kupelekwa sehemu sahihi ili hatua ziweze kuchukuliwa, msijichukulie sheria mkononi," alisema.

Kamanda wa Kikosi cha Afya Tanzania, ACP Hussein Yahya, akizungumza kwa niaba ya kikosi cha afya kilichoko chini ya Kamisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, alishukuru timu ya Kinondoni kwa kutoa msaada huo.

"Tumekuwa na uhitaji wa vifaa kwa muda mrefu na tumekuwa tukipata shida ya upatikanaji wake kutokana na hali halisi ya kibajeti.

"Mmetuongezea nguvu na vifaa hivi vitakuwa sehemu ya kuboresha huduma, kwa asilimia kubwa wahanga wa ukatili wa kijinsia mwisho wa siku hufika hospitali, vifaa hivi ni sehemu ya kuboresha huduma zao ambazo hukutwa na ukosefu wa kifaa vya kutosha," alisema.

Yahya alisema vifaa vya usafi walivyopewa vitasaidia kuhakikisha eneo la hospitali hiyo muda wote kuwa safi.

"Ninaziomba taasisi nyingine kwa kuwa kikosi cha afya kina vituo vingi vya afya nchini na wahanga hufika huko kwa ajili ya kupata huduma tunaomba nao waone haja ya kusaidia," alisema.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na Waumini wa Kiislam baada ya kumalizika kwa Sala ya Ijumaa katika Masjid Istiqaama Shangani mji mkongwe, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Dk. Mwinyi ataka Waislamu kumwombea

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amewaomba Waislamu kuendelea kumuunga mkono na kumwombea dua ili kutekeleza aliyodhamiria kuwafanyia wananchi na apate wepesi wa kuyafanya.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana huko Masjid Istiqama Shangani, jijini Zanzibar wakati akitoa salamu kwa waumini wa Kiislamu baada ya kumaliza sala ya Ijumaa.

Alisema ameanza kufanya kazi na ameona kasoro zilizopo na anataka kuzirekebisha lakini anajua kwamba ni jambo la kawaida iwapo kasoro zitakapoanza kurekebishwa kuna mambo yatajitokeza.

Rais Mwinyi aliyataja mambo mawili yatakayotokea katika hatua hiyo kuwa ni pamoja na wengi watafurahia kwa sababu watanufaika na wachache hawatofurahia kutokana na kwamba walikuwa wakinufaika katika mfumo uliokuwa na makosa, hivyo bila shaka watu hao hawatompenda.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Mwinyi aliwaomba Waislamu wawombee dua ili kutekeleza dhamira yake ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Alisema aliomba nafasi ya urais kwa dhamira ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na kuwaletea maendeleo na kwamba ndani yake havitokosa vikwazo, hivyo kumwomba Mungu kuviondoa ili kutekeleza yaliyomo kwenye dhamira yake. Pia aliwashukuru Waislamu na wananchi wa Zanzibar kwa kukamilisha uchaguzi kwa amani na utulivu na kumwomba Mwenyezi Mungu amani iliyopo izidi kudumu ili kuishi kwa amani na kufanya ibada kwa amani.

Dk. Mwinyi alisema katika kipindi cha uchaguzi alikwenda msikitini hapo na kuwaomba Waislamu na wananchi wote wa Zanzibar kwamba mara nyingi kipindi kama hicho amani huvunjika na matatizo mengi hutokea.

Kwa mantiki hiyo, alisema aliwaomba wananchi wote waendelee kuilinda amani iliyokuwapo na kumuomba Mwenyezi Mungu kwa kujalia kumalizika kwa uchaguzi mkuu kwa salama na amani na kusisitiza kwamba lililobaki hivi sasa ni kuendelea kuijenga nchi.

Alisema nchi hujengwa na wananchi wote na si serikali pekee yake na kutilia mkazo kwamba kila mtu akifanya wajibu wake pale alipo basi nchi itajengeka. Aliongeza kuwa kila pale anapofanya uteuzi wa wasaidizi mbalimbali amekuwa akisisitiza kwamba kila mtu awajibike katika nafasi yake.

Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi wote kila mtu alipo akiwa katika kazi ya serikali, binafsi, ufugaji, mvuvi, ukulima kutimiza wajibu wake na kwa kufanya hivyo, maendeleo ya nchi yatapatikana. Alisisitiza kuwa serikali anayoiongoza inafanya kila linalowezekana kuhakikisha yale yaliyoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi na katika ahadi yanatekelezwa na kwamba ili kufanikisha hayo, kunahitajika mambo mawili likiwamo la kuilinda amani iliyopo.

"Jambo la pili ni kuhakikisha kuwa kila mtu anawajibika katika nafasi yake ya kazi aliyo nayo, kwani iwapo uwajibikaji utakuwapo na kila mtu atawajibika, wakiwamo viongozi wa serikali, hakuna shaka kwamba yote yaliyoahidiwa kwa wananchi yatatekelezwa ikiwa ni pamoja na kuwaletea wananchi maendeleo.

# Wanaswa madai ya kusafirisha binadamu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IDARA ya Uhamiaji katika miezi 11, imewakamata Watanzania 45 wanaodaiwa kujihusisha na biashara ya usafirishaji wa binadamu.

Imesema licha ya kuwakamata watu hao, bado inaendelea kufanya uchunguzi wa kina ili kuwabaini watu wengine wanaojihusisha na biashara hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Dk. Anna Makakala, alisema watu hao wamekamatwa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Novemba, mwaka huu na kufikishwa mahakamani.

Alisema Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 2015 sura ya 54 inatoa adhabu kwa watu wanaojihusisha na biashara haramu ya binadamu, ambayo ni pamoja na kifungo cha miaka 20, faini mpaka Sh.milioni 20, au adhabu zote mbili.

Kamishna huyo alisema tayari sheria imechukua mkondo wake kwa watu hao.

Pia alisema katika kipindi hicho Idara ya Uhamiaji imefanikiwa kuwakamata wahamiaji haramu 15,266 na kueleza kuwa idadi hiyo imechangiwa na baadhi ya Watanzania wasio wazalendo kuwa ndio wahusika wakuu wanao wahifadhi.

"Nitoe onyo kali kwa wananchi ambao wamekuwa wakiendelea na biashara hii haramu ya binadamu tutahakikisha tunawachukulia hatua kwa kuwa inahatarisha usalama wa nchi," alisema Dk. Makakala.

Pamoja na hayo, alisema vyombo vya usafiri vimekamatwa yakiwamo magari 13, boti mbili, pikipiki 16 ambavyo vimekuwa vikitumiwa na wanaofanya biashara hiyo. Kadhalika, alisema Idara hiyo inazo taarifa za kutosha za kiintelijensia kwa wote wanaojihusisha na biashara haramu ya binadamu.

Aliishukuru Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Mahakama kwa ushirikiano mkubwa uliofanikisha kukamatwa kwa wahusika hao, huku akiwaomba wananchi kutoa taarifa endapo watawaona watu wanaofanya biashara hiyo.

"Mgeni akipita anatakiwa kupita kituo rasmi ili kupata taarifa zake, mgeni huyo amekuja kufanya nini nchini, madhumuni ya safari ni nini na taarifa zake binafsi, Pale tunapoona mgeni huyu si salama basi atazuiwa kabla hajaingia hapa nchini," alisema Dk. Makalala na kuongeza:

"Sasa mwananchi yeyote akithubutu kuingiza mgeni ambaye hatujui taarifa zake binafsi na amekuja kufanya nini kwa kupewa hela ndogo anahatarisha usalama wa nchi nzima, ni harari kwa usalama wake binafsi, familia yake,"alisema Dk. Makakala.

Alisema wageni wengi wanaingia hapa nchini wanajihusisha kwenye matukio ya kiuhalifu kama vile ujambazi wa kutumia silaha.

Alisema: "Mipaka yote italindwa na hakuna mtu atakayekatisha sehemu yoyote ilipo kwa maana sasa hivi watu wameanza kujaribu kufika maeneo ambayo walikuwa hawawezi kama Mwanza, Bagamoyo wamekamatwa wengi lakini kwa sababu tupo macho ninawaonya sana na sheria itaendelea kutimizwa kama ilivyo sasa"

HABARI KITAIFA

# Dawasa sasa yajivunia miradi mkubwa Kigamboni, Mkuranga

**Na Beatrice Shayo**

MWENYEKITI wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Jenerali Mstaafu Davis Mwamunyange, amesema miradi mikubwa ya maji katika maeneo ya Mkuranga na Kigamboni iko kwenye hatua nzuri kukamilika.

Kukamilika kwa miradi hiyo, kutawawezesha wananchi kuondokana na kero ya maji iliyowakumba kwa muda mrefu.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya bodi hiyo kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo, kueleza utekelezaji wake unaoendelea vizuri ambao utawafanya wananchi kuanza kupatiwa huduma ya maji katika maeneo hayo.

Mwamunyange alisema mradi huo ni muhimu na utakidhi kilio cha muda mrefu kwa wananchi wa Mkuranga na Kigamboni.

Alisema kwa mradi wa Mkuranga tayari kazi ya uzalishaji wa mabomba ya usambazaji maji imefikia asilimia 97.15 na kazi ya ujenzi wa tanki la maji imefikia asilimia 20.

Pia alisema mradi huo unagharimu Sh. bilioni 5.5 ambazo ni fedha za ndani kwamba ujenzi wa tanki la maji utagharimu Sh.bilioni 2. 602 na gharama ya ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji ni Sh.bilioni 2.597.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema mradi wa Kimbiji ni mkubwa wenye matenki ya Sh. bilioni 10, Pampu za kisima Sh.bilioni 12 na kusambaza maji Sh. bilioni tatu.

Alisema mradi wa maji Kigamboni utakamilika Aprili, mwakani na maeneo ambayo yatanufaika ni Kisarawe, Kibada, Toangoma, Kigamboni, Mji mwema, Vijibweni, Kimbiji na Gezaulole.

Mradi wa Kigamboni unaotekelezwa na serikali kupitia DAWASA, alisema unahusisha uendeshaji wa visima vya maji 12 katika eneo la Kimbiji Wilaya ya Kigamboni na visima vinane katika eneo la Mpera Wilaya ya Mkuranga.

Alisema hadi sasa visima 14 vimechimbwa vyenye urefu wa mita 400 hadi mita 600. Visima saba vya Kimbiji vimeonyesha uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 57 kwa siku na mahitaji ya wananchi wa Kigamboni matumizi yao ni lita milioni 25 kwa siku.



Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Rhoben Nkori (wa pili kulia). akikabidhi cheti kwa mmoja wa washiriki wa mafunzo ya kuwajengea uwezo makandarasi wa ndani yaliyoandaliwa na bodi hiyo kwa Makandarasi wa Nyanda za Juu Kusini, mjini Njombe. Wengine ni Meneja wa CRB Kanda ya Kusini, Mhandisi Ally Mwita (kulia), Mratibu wa mafunzo wa bodi hiyo, Neema Fuime (kushoto) na Naibu Msajili wa Bodi hiyo, David Jere. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC aonya walanguzi pembejeo

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

SERIKALI wilayani Kalambo mkoani Rukwa imewaonya wafanyabiashara wilayani humo wanaouza pembejeo za kilimo kwa bei ya juu, tofauti na bei elekezi ya Sh. 61,000.

Onyo hilo alilitoa jana na Mkuu wa Wilaya hiyo, Carlos Misungwe, wakati akijibu malalamiko ya baadhi ya wananchi waliokuwa wakilalamikia kupanda holela kwa bei ya mbolea kutoka Sh. 61,000 kwa mfuko wa kilo 50 hadi Sh. 71,000.

Alisema wafanyabiashara waliopandisha bei ya pembejeo wanapaswa kushusha haraka kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Misungwe alisema pembejeo hizo zimewekewa bei elekezi na bunge la 11 na mpaka sasa serikali haijatangaza bei mpya. Aliongeza kuwa kwa kuwa hivi sasa ni msimu wa kilimo, kwamba mahitaji ya mbolea yamekuwa juu, hususani mbolea za kupandia na kukuzia, ndiyo maana baadhi ya wafanyabiashara wasio waadilifu wametumia mwanya huo kupandisha bei.

Wakizungumza na Nipashe, mmoja wa wakulima wilayani humo, James Simzosha, alisema hali hiyo imesababisha usumbufu kwa wafanyabiashara wadogo, huku baadhi yao wakilazimika kupanda mazao bila kutumia mbolea.

Alisema suala hilo lisipochukuliwa hatua za haraka na serikali, huenda wakulima wasifanikiwe katika kilimo, kwa kuwa hakuna muujiza wa kupata mazao mengi na bora bila kufuata taratibu za kilimo bora pamoja na matumizi ya pembejeo za kilimo.

Simzosha aliwaomba wakulima wenzake kupaza sauti kwa kutumia njia mbalimbali ili serikali ichukue hatua, hasa ikizingatiwa kuwa kilimo kinakwenda na muda iwapo muda wa kupanda mazao ukiisha na wakalazimika kupanda bila mbolea watakaoumia ni wao wenyewe.

# Wataka kuridhia mkataba wa ILO kutokomeza ukatili

**Na Joseph Mwendapole**

WADAU mbalimbali wameiomba serikali iridhie mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Kazi Dunia (ILO) wa kutokomeza ukatili maeneo ya kazi ili kuwawekea mazingira mazuri wafanyakazi kwa kuondoa ubaguzi na unyanyasaji kwenye maeneo ya kazi.

Walitoa ushauri hao jana wakati wakizungumza kwenye mkutano wa siku moja kujadili namna ya kutokomeza vitendo vya ukatili maeneo ya kazi ulioandaliwa na Sihirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) na kushirikisha vyama vya waajiri, Shirika la Kazi Duniani (ILO) na asasi mbalimbali za kiraia.

Kwa mujibu wa ILO mkataba huo wa ILO C 190 tayari umekubaliwa na mataifa zaidi ya 170 wanachama kama mkataba wa kazi na baadhi ya nchi zimeshaanza mchakato wa kuuridhia.

Devotha Tweve kutoka Young Alive Initiative alisema kuridhiwa kwa mkataba huo kutawapunguzia wanawake unyanyasaji hasa wa kingono ambao umekuwa ukiwakabili kwa miaka mingi.

"Mkataba huu ni muhimu sana kwasababu kila mtu ana haki ya kufanyakazi bila kubaguliwa wala kunyanyaswa katika msingi wowote ule. Wanawake ndio wamekuwa waathiriwa wakubwa kwenye unyanyasaji sehemu za kazi," alisema.

Aidha, Tweve alisema mtu anapoathiriwa na unyanyasaji wa aina yoyote sehemu ya kazi hupata madhara ya kisaikolojia ambayo husababisha ashindwe kutekeleza majukumu yake ya kazini na nyumbani.

"Kuna manyanyaso mtu anapata mpaka anaona bora aache kazi hapo aende akatafute kazi kwingine sasa kwanini tufikie kote huko ndiyo sababu tunaona mkataba huu utakuwa mkombozi hasa kwa wanawake na uzuri ni kwamba mkataba umamlinda aliyeko kazini na asiye kazini" alisema.

Edina Rwezaura wa asasi ya TAMCO alisema kuridhiwa kwa mkataba huo kutasaidia wafanyakazi kuondoa hofu kwani mwajiri atakuwa anajua kuwa kuna mkataba unaolinda haki za wafanyakazi.

Alisema wafanyakazi wengi hasa wanawake ambao ndio wanaonyanyasika zaidi makazini watatambua haki zao hivyo kuongeza ufanisi sehemu zao za kazi.

Kuna watu wanapendelewa kazini kwa sababu tu ya rushwa ya ngono hivyo mkataba huu ukiridhiwa waajiri wataogopa kutoa upendeleo kwa hiyo na hawa ambao hawakuwa wanapata fursa watanufaika," alisema

Aidha, alisema hali hiyo itasaidia sana kuimarisha uhusiano mwema kazini kwani wafanyakazi wote watakuwa sawa mbele ya sheria na hakutakuwa na matabaka, vitendo vya upendeleo wala unyanyasaji.

Hohnbest Mwahaja kutoka Vijana Think Tank alisema kuna umuhimu wa kuhamasisha wafanyakazi kuujua mkataba huo ili wafahamu haki zao kazini zinapokiukwa.

Alisema kuna haja kwa wanaharakati kufanya kila linalowezekana ikiwamo kupasa sauti zao kupitia vyombo vya habari kuhakikisha serikali inaridhia mkataba huo.

"Kuna haja ya kutumia vipeperushi, mitandao ya kijamii ili serikali isikie kilio cha wafanyakazi kote nchini na mwishowe isaini mkataba huu ambao utaleta heshima sehemu za kazi na kupunguza ubaguzi na unyanyasaji hasa wa kingono kazini," alisema.

Alisema kutiwa saini kwa mkataba huo kutawaondolea sonona na wafanyakazi kujiamini kwani watakuwa na uhakika kuwa hawezi kufukuzwa kwa chuki au kutopata haki yake kwa kushindwa kutoa rushwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Namungo bado hamjamaliza kazi CAF

MASHINDANO ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), yanatarajiwa kuendelea tena wikiendi hii katika viwanja mbalimbali hapa barani. Michuano hiyo ya leo na kesho itakamilisha michezo ya marudiano na timu zitakazopata matokeo Bora zitasonga mbele kwa kucheza hatua inayofuata.

Katika mashindano hayo, Tanzania Bara inawakilishwa na Simba inayoshiriki Ligi ya Mabingwa Afrika na Namungo ambao wanapeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Mlandege ya Zanzibar yenyewe inachuana katika kusaka taji la Ligi ya Mabingwa Afrika huku KVZ wenyewe wakipambana kusaka ubingwa wa Kombe la Shirikisho.

Hata hivyo, Simba na Namungo ndio zilipata matokeo chanya katika mchezo wao wa kwanza tofauti na wenzao, Mlandege waliokuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Amaan na KVZ iliyoanzia Sudan zilizokubali kichapo. Simba ilianzia ugenini kwenye Mji wa Jos nchini Nigeria ikipata ushindi wa bao 1-0 na Namungo inayotumia Uwanja wa Azam yenyewe iliondoka na ushindi mnono wa magoli 3-0 dhidi ya Al Rabita kutoka Sudan Kusini.

Licha ya Simba na Namungo kuanza vyema kampeni zao, lakini wanatakiwa kujipanga zaidi kwa kulinda ushindi walioupata kwa sababu hatua hiyo wanaocheza ina dakika 180. Wanacheza dakika 90 za kwanza na zimebakia dakika 90 za mwisho.

Nipashe inawakumbusha kushuka uwanjani wakiwa na lengo moja la kujituma zaidi ili kuondoka tena na ushindi na kamwe wasiingie dimbani wakiwaza kutoka sare, mawazo hayo yanaweza kuwaweka kwenye hali ya hatari. Katika mpira lolote linawezekana, kama timu yako ilipata ushindi katika mchezo wa kwanza, vile vile inawezekana mpinzani wako naye akapata ushindi kwenye mechi hiyo ya marudiano na kubadilisha upepo uliokuwa unavuma.

Wachezaji wa Simba na Namungo hawatakiwi kubweteka, wanatakiwa kukumbuka na kufahamu mpira ni mapambano yanayomalizika baada ya kusikia filimbi ya mwisho ya mwamuzi na si jambo lingine. Tunawakumbusha katika mpira wa miguu hakuna kuridhika na matokeo, kila mechi itumike kusaka ushindi na kuacha kufikiria matokeo ya michezo iliyotangulia.

Nyota wa Simba na Namungo kamwe hawapaswi kuridhika na matokeo yaliyopatikana kwenye mechi ya kwanza, wanatakiwa kushuka uwanjani wakiwa na nguvu mpya kwa ajili ya kukamilisha kazi waliyoianza wiki iliyopita.

Wawakilishi wote wa Tanzania wanatakiwa kuwaheshimu wapinzani wao ili kujiweka katika nafasi ya kupambana, ikumbukwe kama timu yako ilifanikiwa kuanza vyema hata wao wanaweza kupata ushindi na kuwatoa kwenye michuano.

Namungo ambayo imepata bahati ya kucheza nyumbani mechi zote mbili baada ya hali ya usalama kwa wapinzani wao (Al Rabita), kutoridhisha, wanatakiwa kutumia nafasi hii kufanya vizuri lakini wakijiandaa na changamoto za ugenini endapo watafanikiwa kusonga mbele. Gazeti hili linawakumbusha kutowaruhusu wapinzani 'wapindue meza' baada ya kupata nafasi ya kuwasoma kwenye mechi za kwanza na kufahamu ubora na madhaifu ya vikosi vyao tofauti na walivyokuwa wakiwafahamu kabla ya kukutana wiki iliyopita.

Kwa upande wa Mlandege na KVZ, kupoteza mchezo wa kwanza sio mwisho wa mashindano, tunaamini makocha wameshayafanyia kazi makosa yaliyojitokeza katika mechi za kwanza na leo mtashuka uwanjani mkiwa na nguvu mpya za kukamilisha majukumu mliyonayo. Ni vyema timu zote nne zikakumbuka zinapeperusha bendera ya Tanzania hivyo wakati wote wa mchezo wanatakiwa kujituma na kucheza soka la kiwango cha juu.

Mungu ibariki Simba, Namungo, Mlandege na KVZ katika kupeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwanzo ni awali ya tendo

Na Barnabas Maro

**MWANZO** ni awali ya tendo; kiini, chimbuko, chanzo; mwongozo unaoelekeza. "Mwanzo wa ngoma ni lele," yaani uimbaji wa kuanzia ngoma.

Twakumbushwa kwamba mambo yoyote makubwa huanzia madogo. Pia huweza kutumiliwa ugomvi au vita ambavyo hutanguliwa na kutoelewana.

Mchezo ni jambo ambalo watu au timu hulifanya kwa kushindana ili kupata mshindi. Pia ni kazi ya sanaa ambayo huigizwa kwa ajili ya kuelimisha na kuburudisha watu. Jambo ambalo mtu hulifanya kwa kujifurahisha: maonesho kama vile mchezo wa kuigiza; sinema.

"Chuki" ni hali ya kutokuwepo upendo, kuwa na roho mbaya, kuwa na kinyongo; hisia ya kutopenda kitu au jambo. "Chukia" ni kitendo cha mtu kutompenda mwingine; poteza mapenzi; kasirika, nuna.

Ndo maana wahenga walitambua hili mapema hata wakatuachia methali isemayo: "Chuki humchoma anayeihifadhi." Kwa kawaida chuki humsumbua anayeiweka au kuihifadhi. Methali hii yatufunza umuhimu wa kutoweka chuki kwani tunajidhuru wenyewe.

Toleo lililopita niliandika kwenye safu hii kumkanusha msomaji aliyenitumia ujumbe wa simu kwa kunisahihisha kuwa Yanga na Simba sio 'wapinzani wa jadi' kama nilivyoandika, bali ni 'watani wa jadi.'

Msomaji wa gazeti maarufu la michezo nchini aliandika yafuatayo kwenye gazeti hilo akiwa Tengeru mkoani Arusha kabla ya mechi ya Simba dhidi ya Plateau United ya Nigeria:

"Chapeni haooo PLATEAU United ebu jipigieni hiyo mizee ya Msimbazi, irudi nyumbani tuwanyooshe kwenye Ligi Kuu Bara ... Hao jamaa weupe sana mkiwakazia. Tunawasubiri Taifa."

"Yeye asemaye kwamba yumo nuruni, naye amchukia ndugu yake, yumo gizani hata sasa. Yeye ampendaye ndugu yake, akaa katika nuru, wala ndani yake hamna kikwazo. Bali yeye amchukiaye ndugu yake, yu katika giza, wala hajui aendako, kwa sababu giza limempofusha macho." (1Yoh. 2:9-11).

Nachelea (kitendo cha kutofanya jambo kwa kuhofia madhara yake) kuandika jina la aliyetuma maneno ya kuiombea Simba mabaya ili ifungwe ugenini. Nalazimika kulinda usalama wake kutoka kwa wanachama na wapenzi wa Simba wenye misimamo ya ovyo kama yeye! Kumradhi (tamko la upole la kumwomba mtu jambo au msamaha.)

Jina la aliyeandika maneno hayo ni la Kikristo. Hivyo kwa nia njema namshauri, kama ni Mkristo kindakindaki (halisi) asome mistari ifuatayo ya Biblia Takatifu ili ajifikirie na kuomba msamaha kwa Mungu.

Upendo kati ya ndugu: "Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari, haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; hutumaini yote, hustahimili yote." (1 Kor. 13:4-7).

Sijui aliyeandika vile alijisikiaje baada ya Clatous Chama wa Simba kufunga bao pekee dhidi ya Plateau United ya Nigeria, mbele ya maelfu ya wapenzi wao na watazamaji wengine ambao bila shaka walijiuma vidole na kusema: "Khaa!" (tamko la kuonesha kukasirika au dharau) wakisikitika timu yao kupoteza mchezo nyumbani!

Bila shaka wenyeji walijiuliza: "Kama tumefungwa kwenye uwanja wetu wa nyumbani mbele ya wanachama na wapenzi wetu, itakuwaje timu yetu itakapokuwa ugenini jijini Bandari ya Salama kwa Watanzania?"

"Dunia ina hadaa kiumbe jitunze." Maana yake binadamu anapaswa kujitunza asipatikane na madanganyo ya ulimwengu. Methali hii hutumiwa kumnasihi na kumkanya mtu anayeelekea kuyapapia maisha bila kufikiri kuwa ulimwengu unaweza kumhasiri (kitendo cha kumtia mtu hasara) na kuishia kumletea kilio kikubwa.

Swali langu linarudi palepale 'niliposahihishwa' kuwa Yanga na Simba si "wapinzani wa jadi" bali ni "watani wa jadi." Je, Watani wa jadi huombeana mabaya kama mtu huyo wa Tengeru,

Arusha alivyoiombea mabaya Simba ya Tanzania ifungwe ugenini na timu ya Plateau United ya Nigeria?

Tanzania ni nchi yenye makabila 120 na ushei (ziada katika idadi iliyotajwa) na timu mbalimbali za kandanda kutoka mikoa tofauti lakini sote ni wananchi wa taifa moja liitwalo Tanzania bila kujali makabila yetu. Kwa nini tubungudhiane (kitendo cha kukera mtu kwa maneno au vitendo) wenyewe kwa wenyewe? Inasikitisha na kushangaza eh?



Mkuu wa wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mhandisi Mwanasha Tumbo (wa pili kulia), akikabidhi cheti cha pongezi kwa Mwandishi wa habari wa gazeti la Nipashe, Steven William, alichotunukiwa na serikali ya wilaya hiyo, kwa kushiriki kikamilifu kuandika habari za shughuli za maendeleo, wakati wa hafla ya kuhitimu mafunzo ya askari wa jeshi la akiba, wilayani humo juzi. Kulia ni Mshauri wa jeshi la akiba wilaya hiyo, Luteni Kanali Charles Madeghe na (kushoto) ni Diwani wa kata ya Tongwe, Erasto Mhina. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CTI yajitia kitanzi mikopo viwanda vidogo

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), limeahidi kuendelea kuwatafutia fursa wajasiriamali wenye viwanda vidogo ili kupata mikopo itakayowawezesha kukuza mitaji yao na kuanzisha viwanda vikubwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodegar Tenga, alitoa ahadi hiyo juzi wakati akifungua kongamano la siku moja kuhusu namna ya kuwapatia mitaji wafanyabiashara wadogo.

Alisema nchi imefikia uchumi wa kati lakini ilikwenda mbali zaidi na kufika uchumi wa juu kwa haraka hakuna namna ya kukwepa wajasiriamali wadogo maana wao ndio msingi wa kufikisha uchumi juu.

Wajasiriamali wadogo, alisema ndio msingi wa biashara kubwa na viwanda vikubwa kwani watu wote wanaoonekana wakubwa leo walianza wakiwa wadogo na walipowekewa mazingira mazuri walikua na kufanikiwa zaidi.

Alisema kwa sasa nchi imejikita kwenye uchumi wa viwanda hasa kuinua biashara ndogo ndogo ili ziweze kukua na kuzalisha ajira kwa wingi.

"Ili kuchochea uchumi wa viwanda lazima tukazanie wafanyabiashara wadogo sasa ili hawa wakue lazima uwawekee mazingira mazuri ya kupata mitaji na mitaji ni kuwawezesha kupata mikopo," alisema.

Alisema viwanda vidogo na vya kati ndivyo ambavyo vinachukua asilimia 97 ya viwanda, hivyo kuna ulazima wa kuvisaidia kuviinua vikue na viweze kuchangia pato la taifa. "Ndiyo maana tunawakutanisha na wataalamu wawape mafunzo namna ya kupata fedha za mitaji kwa kukopa benki na tunawasaidia kupata masoko tunawakutanisha na wataalamu wa masoko waonyeshwe maeneo muhimu ya kuuza bidhaa zao," alisema Tenga.

Alisema CTI ina dawati maalum kwa ajili ya kukutana na wanachama na kuwapa elimu kwamba mtaji si fedha tu bali elimu inapaswa kupewa kipaumbele kwa mfanyabiashara anayeanza na aliwakaribisha wafanyabiashara.

Alisema CTI imekuwa ikiwapa taarifa muhimu za biashara za ndani na nje ya nchi ili wafanyabiashara hao wajue mazingira ya sasa ya biashara ya maeneo hayo wanapopeleka bidhaa zao.

"Tunaendelea kuwapa taarifa nyeti maana kuna sera za biashara zinabadilika, kuna mabadiliko ya sheria nchi kadhaa ni CTI ambayo tunawaambia wafanyabiashara ili waende na wakati na tunafanya hivyo ili wajidhatiti na waweze kushindana na wenzao," alisema.

# Mbunge asema hatalala usingizi

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MBUNGE wa Kilolo mkoani Iringa, Justine Nyamoga, amesema baada ya kuchaguliwa na wananchi kuwatumikia, anakwenda bungeni kuchangia hoja za kuleta maendeleo na si 'kuuchapa' usingizi.Amesema hatakubali kuona mtumishi wa serikali akifanya kazi kwa mazoea na kushindwa kuwatumikia wananchi.

Aliyasema hayo kwenye mahojiano maalum na mojawapo ya chombo cha habari mkoai Iringa, kueleza kuwa lazima afanye kazi kama wananchi walivyomuamini, pamoja na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Kazi kubwa niliyopewa na wananchi ni kuwatumikia katika kuwaletea maendeleo na kushughulikia kero zao, kwa sababu tuliomba wenyewe, naomba madiwani wafanye kazi na mimi, kamwe hatutamuangusha Rais John Magufuli," alisema Nyamoga.

Alisema tangu alipochaguliwa kuwa muda amefanya shughuli mbalimbali ikiwamo kuteua watendaji watakaomsaidia katika kazi zake za kibunge, akiwamo dereva na makatibu wawili.

Alisema pia amekutana na wakuu wa idara mbalimbali wakiwamo wa taasisi binafsi na mashirika.

Nyamoga alisema akiwa katika ziara za kiubunge, alifarijika kuona kazi kubwa iliyofanywa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) katika kusambaza umeme vijiji.

Alisema katika sekta ya maji nako kumefanyika kazi kubwa, kwamba wananchi wamepata huduma hiyo wakiwamo wa Ruaha Mbuyuni ambako kuna mradi wa maji katika kijiji cha Msosa unajengwa.

Alisema kata ya Lugalo kuna mradi wa maji unajengwa na ipo miradi mingine 11 inayoendelea kujengwa Kilolo, ambayo itamaliza kero ya upatikanaji wa maji.

Mbunge huyo alisema, kuna vijiji vichache ambavyo vinahitaji miradi mipya ya maji.

Hata hivyo alisema kuna vijiji vichache ambavyo vinahitaji miradi mipya ya maji.

Kuhusu ubovu wa barabara, Nyamoga alisema serikali inaendelea kufanya matengenezo ya barabara hususani maeneo korofi, kwa kuweka lami na kumwaga kifusi.

Kadhalika, Nyamoga alisema ataendelea kutoa mrejesho kila wakati kwa wananchi kuhusu maendeleo aliyoyafanya ili waweze kumpima pamoja na kutekeleza ilani ya CCM.

# Wananchi wachangishana fedha ujenzi kituo afya

**Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Kata ya Mapamba, Halmashauri ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga, wamechanga Sh. milioni 6.8 kwa ajili ya kujenga kituo cha tiba na matunzo kwa wananchi wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU).

Harambee hiyo ilifanyika juzi na kuongozwa na Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani.

Maadhimisho hayo kimkoa yalifanyika katika kata hiyo na kuhudhuriwa na wananchi mbalimbali.

Ndanya alisema fedha hizo zilichangwa na wananchi wa kata hiyo kwa kushirikiana na uongozi wa wilaya na mkoa.

Pia alisema licha ya kata hiyo kuwa na zahanati, bado wananchi wanalazimika kutembea umbali wa kilomita 10 kwenda kituo cha afya cha Ukune, zahanati za Busenda, Uyogo na Chambo kupata huduma za afya na kuchukua dawa za kufubaza VVU.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu, Dk. Senguo Nicodemus, alisema kukamilika kwa jengo hilo katika kata ya Mapamba kutasaidia kuongeza mahudhurio ya wagonjwa hasa wa VVU na Ukimwi.

Pia alisema itasaidia wananchi kutoendelea kutembea umbali mrefu 10 kwenda katika vituo na zahanati za jirani kupata huduma hiyo.

Alisema huduma ya tohara kwa wananchi wa Halmashauri hiyo katika kata zote 20 imesaidia kupunguza maambukizi ya VVU kwa asilimia tatu na kwamba bado wanaendelea kutoa elimu kwa vijana na watu wazima kuendelea kufanya tohara.

Kuanzia Januari hadi Novemba, mwaka huu, alisema waliwapima VVU kwa hiari zaidi ya wananchi 32,000 na kwamba kati ya hao 12,000 waligundulika kuwa na maambukizi na wote waliandikishwa na kuanzishiwa dawa katika vituo vya afya vya jirani.

Aliwataka wananchi kuwa wawazi kwa mwenza wao endapo watapima na kubainika kuwa na VVU ili kuwalinda na kuwahamasisha vijana kujitokeza kwa kufanyiwa huduma ya tohara kujikinga na maambukizi na kumkinga mwenza na saratani ya shingo ya mlango wa kizazi.

# Majaliwa akoleza moto bidhaa hafifu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI mkuu Kassim Majaliwa, ameziagiza mamlaka zote za udhibiti kuhakikisha bidhaa zinazoingizwa nchini kwa ajili maonyesho mbalimbali zinakuwa na viwango vya kimataifa.

Pia amesema bidhaa zisizo na viwango na bidhaa bandia hazitapata nafasi ya kuingia kwenye soko la Tanzania na kuwataka wamiliki wa viwanda wazalishe bidhaa kwa wingi na kwa kutumia malighafi zinazopatikana, hivyo kuwa na uzalishaji wenye gharama ndogo na kuwa na bei shindani katika soko.

Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo jana baada ya kufungua Maonyesho ya Tano ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania katika Uwanja wa Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa wa Mwalimu J. K. Nyerere, Dar-Es-Salaam. Kaulimbiu ya maonyesho hayo ni 'Tumia Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania.'

"Watanzania tuachane na fikra potofu kuwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi ndizo zenye ubora kuliko za hapa nchini kwani bidhaa zetu ni bora na zina viwango vinavyostahili.

"Hebu sote tununue bidhaa zetu ili kukuza ajira na pato la mtu binafsi na taifa kwa ujumla. Sisi Watanzania tunazalisha vitu bora na vyenye uhalisia," alisema Majaliwa.

Amesema uwekezaji unaofanywa lazima uzingatie uendelevu, ubora na tija kulingana na viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa katika shughuli za uzalishaji ili kuhimili ushindani na hata kunufaika na fursa za masoko zinazoendelea kujitokeza.

"Nina hakika tukijipanga tutaweza kuwa washindani mahiri na bidhaa zenu zitaingia na kuleta ushindani mkubwa kwenye soko," alisema. Pia Waziri Mkuu aliwataka wawekezaji na wazalishaji wote nchini wafanye biashara halali, walipe kodi kikamilifu na wahakikishe watanzua kumbukumbu vizuri ili kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi za biashara zinazofanyika ikiwamo na nchi jirani na kuandaa sera mahususi za kuwasaidia.

"Wizara ya Viwanda na Biashara hakikisheni wazalishaji wanatumia vizuri sheria za uasilia wa bidhaa ili kuweza kukidhi matakwa na kutumia fursa ya masoko ambayo Serikali yetu imesaini mikataba ya maridhiano hususani soko la Afrika Mashariki, SADC, AGOA na fursa nyingine za masoko ya pamoja."

Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kuziagiza halmashauri zote nchini zihakikishe viwanda vilivyo katika mamlaka zao vinashiriki kuonesha bidhaa wanazozalisha ili bidhaa hizo kutafutiwa masoko katika nchi mbalimbali duniani zikwamo nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na kusini mwa Afrika kwa lengo la kuongeza mauzo ya Tanzania nje ya nchi.

Pia Waziri Mkuu aliiagiza Wizara za Fedha na Mipango na Viwanda na Biashara kuendelea na mikakati ya kisera na kikodi ya namna ya kupunguza uagizaji wa baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nje na kuongeza ununuzi wa bidhaa zinazozalishwa ndani ili kukuza viwanda vya ndani mfano; bidhaa za mbao, mafuta ya kula na saruji.

"SIDO (Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo) kwa kushirikiana na VETA (mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi) wekeni kipaumbele cha kutoa mafunzo na kubuni nyenzo zinazoendana na mahitaji makubwa yaliyomo katika jamii ikiwamo katika eneo la kuchakata mazao kama korosho, chikichi, ufuta, alizeti na matumizi ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) katika kuboresha uzalishaji mali, ufanisi, viwango na kutafuta masoko," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) kufanya maboresho katika uratibu wa maonyesho mbalimbali ya viwanda na biashara ili yafanyike kwa kuzingatia kanda za uzalishaji badala ya nguvu kubwa kuelekezwa Dar es Salaam na miji mikubwa.



Kijana Johnbest Mwahaja kutoka asasi ya Vijana Think Tank, akizungumza kwenye kongamano la kutokomeza ukatili wa kijinsia lililoratibiwa na Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mfumo utumishi wa umma sasa kidigitali

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeandaa mfumo mahsusi wa kielektroniki wa Mpango wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma (e-HRP), utakaoziwezesha taasisi za umma kusimamia rasilimali watu vizuri, pamoja na kupata takwimu sahihi za mahitaji ya watumishi wake.

Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Francis Michael, aliyasema hayo wakati akifungua kikao kazi cha wadau kilicholenga kujadili mahitaji ya mfumo wa kielektroniki wa e-HRP.

Dk. Michael alisema mfumo huo utawezesha kubaini mahitaji sahihi ya rasilimali watu kwa sasa na baadaye ili kuwa na mipango mahususi ya kiutumishi, pamoja na matumizi mazuri ya rasilimali watu.

Alisema matumizi ya mfumo huo utaziwezesha taasisi za umma kuwa na watumishi wa kutosha, wenye sifa na uwezo unaotakiwa mahali pa kazi katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi zao.

Aidha, alieleza Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2008, imeelekeza kila taasisi ya umma kuwa na mpango wa kati na wa kila mwaka wa rasilimali watu, kulingana na malengo yake.

Alisema kikao hicho kitaiwezesha serikali kupata maoni ambayo yataboresha mfumo huo katika utumishi wa umma.

## Kampuni yasimamisha uzalishaji magazeti

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya New Habari 2006 LTD inayozalisha magazeti ya Mtanzania, Rai, Bingwa na Dimba, imetangaza kusitisha kwa muda uzalishaji wa magazeti yote kutokana na mwenendo mbaya wa biashara.

Akizungumza na wafanyakazi wa kampuni hiyo jana, Mhariri Mtendaji, Dennis Msacky, alisema hatua hiyo inakwenda sambamba na upunguzaji wa wafanyakazi, ambapo miaka miwili iliyopita ilifanyika na wafanyakazi 150 walipunguzwa.

Msacky alisema uzalishaji wa magazeti hayo utasitishwa kwa muda kuanzia Desemba 7, mwaka huu.

"Usitishaji huu ni wa muda lengo tunahitaji kujipanga vizuri zaidi. Tunajua wasomaji wetu watahoji kwa nini ila ninaomba waelewe ni usitishaji wa muda," alisisitiza Msacky.

Hata hivyo, alisema wakati wote ambao magazeti yatakuwa hayachapishwi, Mtanzania Digital na mitandao yote ya kijamii itaendelea kuwa hewani kuhabarisha umma.

## DC atangaza kusitisha fedha

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MKUU wa Wilaya ya Bukoba, Deodatus Kinawilo, ameagiza makandarasi wote wanaotekeleza miradi ya serikali, kutolipwa fedha zote wanazodai mpaka ufanyike uchunguzi ili kubaini kama wameshawalipa vibarua wanaosaidia kazi.

Kinawiro alitoa agizo hilo jana huku akiwataka wakurugenzi wa Manispaa ya Bukoba na Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, kutekeleza suala hilo ili kuhakikisha vibarua wanapata hazi zao.

Akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu katika shule za sekondari za Nyakato na Rugambwa, Kinawilo alisema amechoka kupokea maandamano ya wananchi wanaolalamikia kupewa kazi na makandarasi na baadaye kuondoka bila kuwalipa na kudai kuwa tabia hiyo inaitia doa serikali.

Mkuu huyo wa wilaya alisema serikali inatimiza wajibu wao kwa kuwalipa makandarasi fedha zao, lakini wao wanashindwa kuwalipa waliowaajiri kama vibarua na kutoa mfano wa mkandarasi aliyekarabati majengo ya shule ya sekondari Rugambwa ambaye mpaka sasa hivi anasakwa.

"Kwa sababu tulijua tabia yake, tuliita mpaka polisi kwenda kumlipa ili tumbane awalipe vibarua, lakini sijui alitutorokaje mpaka sasa tunapata tetesi eti yuko Morogoro, nimewaambia polisi wamsake popote pale alipo akamatwe aletwe huku," alisema.







Spika wa Bunge, Job Ndugai (katikati), akifurahia jambo, baada ya kuwasili katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Walemavu na Shirikisho la Vyama Vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), wilayani Kongwa, mkoani Dodoma juzi. Nyuma yake ni Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto. **PICHA: BUNGE**

# Wawekezaji Austria waonyesha nia ya kuwekeza miradi Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMPUNI za uwekezaji 13 kutoka Austria, zimetua jijini Dodoma kwa ajili ya kutafuta maeneo ya uwekezaji katika sekta za usafirishaji, elimu, kilimo, afya na ujenzi wa miundombinu.

Akizungumza baada ya kufanya mazungumzo na wawekezaji hao, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema katika kikao hicho wamefanya mawasilisho kwa pande zote na jiji limeonyesha maeneo muhimu na fursa zilizopo.

"Leo (jana) tumepokea ugeni mzito kutoka Austria wakitafuta maeneo ya uwekezaji. Tumepata muda wa kila mtu kuwasilisha kwa upande wake wenyewe wakituonyesha maeneo watakayowekeza na wenzetu jiji wakaonyesha fursa zilizopo pamoja na maeneo ya kuwekeza," alisema.

Dk. Mahenge alibainisha kuwa wawekezaji hao wameonyesha nia ya kuwekeza katika maeneo hayo jambo ambalo ni muhimu kwa Mkoa wa Dodoma kwa kuwa ni makao makuu ya nchi.

"Uzuri ni kwamba hata wao walipokuwa wanakuja walifahamu kuwa Dodoma ni makao makuu kwa hiyo hata fursa wanazotaka kuwekeza zimelenga katika ujenzi wa miondombinu na huduma za kijamii katika mkoa wetu," alisema.

Alisema Dodoma ni jiji linalojengwa karne ya 21 na litakuwa la kisasa na linalopangiliwa vizuri.

"Hapa Dodoma tuna hospitali chache sana kuna huduma ukizikosa katika Hospitali ya Benjamini Mkapa inabidi utoke nje ya mkoa kufuata huduma hizo. Kiujumla, hospitali ni chache sana lakini unapopata wawekezaji kama hawa tunaamini tutapata huduma za uhakika na kuweka viwanda vya dawa," alisema.

Alisema miongoni mwa fursa nyingine wanazotafuta wawekezaji hao ni usafirishaji hasa wa treni zinazotumia nishati ya gesi na ni gharama nafuu ukilinganisha na usafiri wa sasa unaotumia mafuta ambayo sio rafiki kwa mazingira.

Mkuu wa Mkoa asema pia upatikanaji wa zao pekee la zabibu katika Mkoa wa Dodoma ni bidhaa zake ni nzuri ikilinganishwa na zinazozalishwa katika maeneo mengine.

"Hapa kwetu nimewaeleza kuna zabibu ambazo ni tofauti na kwingine yaani ina radha ya kipekee kabisa, kwa hiyo nimewakaribisha kuona namna ya kuwekeza katika viwanda vinavyozalisha bidhaa za zabibu," alisema.

Balozi wa Austria wa nchini Kenya, Christian Fellner, alisema wana mradi wa mabasi ya kijani ambayo yanatumia teknolojia ya nishati ya gesi isiyoharibu mazingira. Haya mabasi yana uwezo kubwa kupunguza uchafu wa mazingira na hata vifo kwa asilimia 80. Lakini pia yana uwezo wa kubeba watu wengi tofauti na magari ya mwendo kasi bila kuathiri abiria waliopo," alisema Balozi Fellner.

Alisema mradi huo endapo utafanyika madereva na mafundi 100,000 watapatiwa mafunzo hivyo kuongeza ajira kwa vijana.

Naye Balozi wa Tanzania nchini Kenya, John Simbachawene, aliwashukuru wawekezaji kwa nia yao ya kuwekeza katika jiji la Dodoma ili kuufanya mji huo kuwa bora kama ilivyo miji mingine.

# Wafurahia TEHAMA kurahisisha masomo

**Na Vincent Mpepo,** OUT, DODOMA

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (CKHT) Kituo cha Dodoma, wamesema matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwenye chuo hicho yamesaidia kujifunzia ipasavyo huku wakitekeleza majukumu ya waajiri wao.

Wakizungumza juzi kwenye mafunzo elekezi ya matumizi ya mifumo hiyo na namna ya kujisomea kwa wanafunzi wa mwaka wa masomo 2020/21, walisema mfumo wa chuo hicho wa matumizi ya TEHAMA umewapa fursa ya kujifunza zaidi.

Mwanafunzi wa shahada ya sanaa katika mawasiliano ya umma, Sara Jonas, alisema mifumo ya kujifunzia inayotumiwa na chuo hicho ni mizuri kwa kuwa inatoa fursa ya mwanafunzi kusoma huku akitimiza majukumu mengine kama ni mwajiriwa na amejiajiri katika sekta binafsi.

"Matumizi ya TEHAMA katika kujifunza ni kitu chema kwa kuwa hakiwezi kukatisha kazi au shughuli niifanyayo, iwe ni ajira rasmi au isiyo rasmi," alisema.

Kupitia mafunzo elekezi, alisema wamejua namna ya matumizi ya mifumo ya TEHAMA ya CKHT ikiwamo SARIS, MOODLE na program tumizi ya zoom ambayo hakuifahamu kabla ya mafunzo hayo.

Naye mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika ustawi wa jamii, Aneth Mwambya, alisema kutokana na utandawazi, matumizi ya TEHAMA kwenye vyuo yanatakiwa kuwa makubwa kwa kuwa yanamsaidia mwanafunzi kujiandaa vyema kimasomo.

"Mafunzo yalikuwa mazuri ila kwa maoni yangu kulikuwa na maandalizi duni kwa upande wa vifaa, eneo na wanafunzi wenyewe katika mafunzo hayo japo siku iliyofuata mambo yalienda vizuri," alisema.

Aidha, alisema tatizo lingine ni ugeni wa wanafunzi wengi katika teknolojia ya mawasiliano inachangia kuchelewa kuelewa kwa haraka matumizi ya mifumo hiyo.

Alikiri kuwa mafunzo hayo yamekuwa fursa iliyosaidia kuwajengea uwezo wanafunzi wengi kuhusu mifumo ya usomaji, usajili wa kozi na mitihani.

Mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika elimu CKHT, Rehema Asimwe, alisema uendeshaji wa mafunzo na utoaji wa elimu wa CKHT ni kitu kizuri iwapo mwanafunzi husika atakuwa na uelewa juu ya matumizi ya TEHAMA.

"Ni fursa pekee inayopatikana na kumsaidia mwanafunzi kuingia katika ulimwengu wa TEHAMA kwani ni lazima atajifunza ili kwenda sawa na wenzake katika ujifunzaji, ushiriki na kutoa mrejesho ikibidi kufanya hivyo," alisema Asimwe.

Naye Mtaalamu wa TEHAMA wa Chuo hicho, Hassan Mwazema, alisema mifumo hiyo ni rahisi na rafiki kimatumizi hivyo kuwataka waitumie ili kukidhi mahitaji ya kitaaluma.

Aliwakumbusha umuhimu wa kushiriki kikamilifu kwenye mafunzo hayo ili kujisajili wenyewe badala ya kutumia watu wengine jambo ambalo si salama kwao.

# Wachimbaji wanawake walia na vifaa hafifu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Wanawake Wachimbaji Madini Tanzania (TAWOMA), kimeiomba serikali kuwasaidia vifaa vya kisasa kwa ajili ya shughuli za uchimbaji ili kuondokana na matumizi ya zana duni.

Mwenyekiti wa TAWOMA, Gilly Raja, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye mkutano mkuu wa chama hicho pamoja na uzinduzi wa duka la kuuza bidhaa zitakazo na madini.

Alisema kuwa kinamama wachimbaji madini nchini wanakabiliwa na ukosefu wa vifaa vya kisasa pamoja na milipuko hali ambayo inasababisha washindwe kufikia malengo yao.

"Moja kati ya kero kwetu kinamama wachimbaji madini nchini ni ukosefu wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuchimba madini wengi wanatumia vifaa duni kama vile nyundo na vinginevyo ambavyo havileti tija tunayoihitaji," alisema Raja.

Aidha, aliziomba halmashauri nchini kuwatambua kinamama wachimbaji wa madini na kuwawezesha mikopo isiyokuwa na riba ambayo wataitumia kupata vifaa vya kisasa.

"Halmashauri bado hazijawatambua kinamama hawa ili kuwasaidia kujikwamua kutoka katika hali hii waliyonayo sasa na kuwa wachimbaji wakubwa," alisema Raja.

Katibu Mkuu wa TAWOMA, Salma Kundi, alisema mikakati ya chama hicho ni kupunguza umaskini kwa wanawake nchini kwa kubuni miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kundi alisema pamoja na mikakati hiyo, bado wanakabiliwa na tatizo la uongezaji wa thamani katika madini wanayo yachimba.

Awali, Kamishna wa Madini, Mhandisi David Mulabwa, alisema serikali bado ina mikakati ya kuweka mazingira wezeshi kwa wachimbaji wadogo pamoja na wanawake.

"Hapo zamani moja ya tatizo ilikuwa ni ukosefu wa masoko lakini hivi sasa serikali imejitahidi kila sehemu kumekuwa na soko la uhakika kwajili ya madini haya," alisema.

Alitoa rai kwa benki nchini kutafuta namna sahihi ya kuwakopesha vifaa vya uchimbaji wa madini wachimbaji wadogo pamoja na wanawake.

Kuhusu uzinduzi wa duka la kuuza bidhaa zitakano na madini yaliyoongezwa thamani, Kamishna huyo alisema ni matumaini yake kuwa litasaidia kuongeza mapato katika chama hicho.





## Ahimiza fursa wenye ulemavu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema watu wenye ulemavu wanaweza kufanikiwa kimaisha kama watu wengine kwa kuzitumia fursa zinazotolewa na serikali na mashirika.

Amesema fursa hizo iwapo zitatumiwa ipasavyo, zitabadilisha maisha yao kuwa bora zaidi.

Katika kuhakikisha azma hiyo inafanikiwa, alisema serikali ya Zanzibar inaelewa ukubwa wa tatizo la ulemavu na imejipanga kupambana nalo kwa njia mbalimbali ikiwamo kuwapatia haki na fursa watu wenye ulemavu ili kumudu vyema mazingira yao.

Akizungumza juzi kwenye Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu Duniani katika ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, visiwani hapa, Hemed alisema suala la kuielimisha jamii kuachana na mitazamo hasi juu ya ulemavu ni la msingi.

Hemed alisema elimu hiyo itakwenda sambamba na kupitiwa kwa sheria, sera na miongozo ili watu wenye ulemavu waendelee kupatiwa haki zao za msingi kama wanavyopata watu wengine.

Alisema kwa vile mwelekeo wa taifa tayari umeshajikita kuimarisha uchumi wa buluu, taasisi na jamii zinapaswa kuwashirikisha kikamilifu watu wenye ulemavu katika masuala yote kwenye sekta hiyo ili nao watoe mchango wao kwa taifa.

Makamu wa Pili huyo alisema idadi ya watu wenye ulemavu inaongezeka kila siku kwa sababu ya kasi ya maradhi ya kisukari na shinikizo la damu, yanayosababisha wakati mwingine mtu kupooza au kupoteza viungo vyake.

Alisema kwa Zanzibar, idadi ya watu wenye ulemavu inakadiriwa kufikia 8,265 kati yao wanawake 3,890 na wanaume 4,375. Alisema kwa utafiti wa wataalamu, kuna uwezekano wa kuongezeka kwa idadi hiyo kutokana na sababu ya kuzidi kwa maradhi yasiyoambukiza.

Hemed alisema kasi ya ongezeko la ulemavu inayotokana na maradhi yasiyoambukiza inaweza kupungua kwa watu kufuata ushauri wa madaktari ikiwamo kutumia vyakula vya asili kama mboga, matunda na kufanya mazoezi.

Akiwasilisha risala ya watu wenye ulemavu, Mwakilishi wa Shirikisho la Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar (SHIJUWAZA), Ali Omar, alisema ili kuwasaidia watu wenye ulemavu kupitia mfumo wa uchumi wa buluu ni kulijengea uwezo kundi hilo kwa kutengewa bajeti maalum itakayokidhi mahitajiyao.

# Mwinyi apongeza NBC kusaidia afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amesema gari maalum la kuchukulia wagonjwa lililotolewa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBCO litasaidia kuharakisha upatikanaji wa matibabu hasa kwa kinamama na watoto.

Alisema gari hilo litaharakisha juhudi za kupambana na vifo vya kinamama na watoto na kufanikisha kupatikana kwa ufumbuzi wa uhakika.

Akizungumza juzi na uongozi wa benki hiyo Ikulu mjini Zanzibar, Dk. Mwinyi aliipongeza benki hiyo kwa kushirikiana na serikali katika kuimarisha sekta mbalimbali za maendeleo na kukuza uchumi wa nchi.

Pia alipongeza azma ya benki hiyo ya kuunga mkono juhudi za serikali katika kuimarisha sekta ya afya na kuutaka uongozi wanapotaka kutoa misaada yao ni vyema wakakutana na wataalamu wa sekta wanayotaka kuiunga mkono ili iwe rahisi katika kufikia malengo waliyoyakusudia.

Hata hivyo, alisema amefarajika kwa utayari wa benki hiyo katika kuunga mkono juhudi za serikali na kusisitiza kwamba ushirikiano wa hali ya juu wataupata kwa kuwa lengo ni kuwahudumia wananchi.

Alisema hatua hiyo itasaidia katika kuendeleza yale yote ambayo walielezwa wananchi wakati wa kampeni ili kuyafanyia kazi na kuhakikisha wananchi wanapata faraja katika kutimiziwa ahadi zilizotolewa.

Aliongeza kwamba hivi sasa serikali iko katika kutayarisha maeneo ya ndani na nje na baadaye kuyapambanua yale ya kushirikiana na sekta binafsi na yale ya kushirikiana na sekta ya umma.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, alisema wako tayari kuunga mkono juhudi za serikali kwa kuanza kutoa mchango kwa kuipa Wizara ya Afya gari la kubebea wagonjwa na kuchangia dawa za binadamu.

Alisema ni utaratibu uliowekwa na NBC kutoa huduma za afya kwa kupitia gari kusaidia jamii kwa kuwasaidia wagonjwa kuwapeleka hospitalini katika mikoa mbalimbali ya Tanzania jambo ambalo wameona haja ya kutoa huduma hiyo kwa upande wa Zanzibar.

Sabi alisema miongoni mwa kazi za benki hiyo ni kutoa huduma za kliniki za biashara kwa wafanyabiashara wakubwa na wale wa kati kupitia ushirikiano huo kati ya ubia wa benki na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), kutoa huduma mbalimbali za ukusanyaji fedha na huduma zingine za kibenki kwa wateja na utoaji wa mikopo na mafunzo kwa wajasiriamali sambamba na kutoa elimu ya kibenki.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kulia), akizungumza na mmoja wa wafanyakazi wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, alipofanya ziara maalum kwenye tume hiyo, Shangani jana. **PICHA: OMPR – ZNZ**

# Wabainisha upungufu sheria dhidi ya ukatili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU wa ukatili wa kijinsia leo watazindua upungufu uliomo katika sheria zinazohusiana na ukatili wa kijinsia ikiwa ni sehemu ya vuguvugu la kupinga vitendo hivyo Zanzibar.

Kongamano hilo ni mfululizo wa kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia na litafanyika katika ukumbi wa watu wenye ulemavu, Kikwajuni Weles, kisiwani hapa.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi ya Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema wadau hao walipitia sheria saba zinazohusiana na masuala hayo.

Mbali na TAMWA, aliwataja wadau wengine kuwa ni Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Jumuiya wa Wanawake Wenye Ulemavu (JUWAUZA) na Mtandao wa Kijinsia Zanzibar (ZGC). Alisema katika kuchambua sheria hizo, walibaini kuwa zinakinzana jambo ambalo linasababisha kukwama kwa kesi za udhalilishaji katika vyombo vya sheria au kupata hukumu ndogo.

Alisema sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Adhabu Na. 7 ya mwaka 2018, Sheria Ushahidi Na. 9 ya mwaka 2017, Sheria ya Mtoto Na. 6 ya 2011, Sheria ya Elimu Na. 6 ya 1982, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Na. 6 ya 2018, Sheria ya Mahakama ya Kadhi Na. 6 ya 2017 na Sheria ya Kumlinda Mwari na Mjane Na. 4 ya 2005.

Mzuri alisema kongamano hilo litatoa nafasi kwa washiriki kujadili mapendekezo na nini kifanyike katika hatua za kuboresha sheria na utendaji wa taasisi husika katika kupunguza wimbi la ukatili wa kijinsia.

"Vitendo vya ukatili wa kijinsia vinaendelea kushamiri na bado kwa mujibu wa takwimu watu wanaopata hukumu ni kidogo sana. Kwa mujibu wa taarifa ya Jeshi la Polisi, kuanzia Januari, mwaka jana hadi hadi Agosti, mwaka huu, malalamiko 821 ya ubakaji na ulawiti yameripotiwa lakini ni kesi nne tu hadi sasa ndizo zilizopatiwa hukumu," alisema.

Alisema hali hiyo inaonyesha upungufu mkubwa katika sheria na utekelekezaji wake na hutoa mwanya kwa wabakaji kukimbia makosa yao, hivyo kuendeleza tabia hiyo mbaya.

Maadhimisho ya Siku 16 za kumpinga ukatili wa kijinsia hufanyika kila mwaka kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10.



BEN POL

UKURASA 12





TIMBWILI ZITO

# Mtoto wa Harmonize shakani, liwe jua au mvua haiwezekani

MAMBO si shwari kwa Mwanamuziki maarufu nchini, Harmonize, baada ya watu kuanza kuhoji ukweli wa uhalali wa mtoto aliyemtambulisha kuwa ni wake.

Mwanamuziki huyo juzi alimtambulisha mtoto wake wa kwanza wa kike Zulekha Kondegirl, huku akimuomba msamaha mke wake Sarah Michelloti kwa kupata mtoto nje ya ndoa yao.

Hata hivyo, timbwili liliibuka baada ya mke wake kumjibu kupitia ukurasa wake wa Istagram kwamba Harmonize amejipa mtoto ambaye sio wake.

Kutokana na majibu hayo, baadhi ya watu katika mitandao ya kijamii walibaki na maswali mengi kuhusu uhalali wa mtoto huyo, wengine wakimtaka Sarah kupasua ukweli nani baba wa mtoto huyo.

Katika majibu aliyomwandikia Harmonize, Sarah ameandika "Mungu wangu watu kweli wamevurugwa, mara mbili wamepima DNA ya mtoto bado majibu ni Negative, ila kwa kuwa umeshindwa kupata mtoto umeamua kujipa mtoto asie wako?"

"Hongera kwa adoption (kuasili), utakua na roho nzuri hukujua jinsi ya kutunza mke sababu ya maovu yako natumai utajua kutunza mtoto, ukome kuongopea mashabiki dah, nimepost hii kwa lugha ya kiswahili kila mtu ataelewa".

Awali, Harmonize kupitia ukurasa wake wa Istagram alimtambulisha rasmi Zulekha katika familia yake na kueleza furaha yake kwa kupata mtoto huyo aliyempata kwa mzazi mwenziye Nana Shanteel.

"Kweli humuweka yeyote huru haijalishi ni kiasi gani au muda gani ila naamini kusema hili litafanya moyo wangu uwe huru na nijione muungwana mbele ya Mungu na wewe unayesoma, pia muungwana zaidi mbele ya mtoto wa wangu kipenzi Zuu, nianze kusema samahani kwa kutojivunia wewe kwa mwaka mmoja na miezi saba"

Akaongeza "Nisamehe pia kwa kutokuwa na muda hata wa kuja kukuangalia pale ulipokuwa unaumwa, kwa kuhofia kuvunja mahusiano ambayo naheshimu sana, tumepitia mengi na naamini kuchezea wanawake au kubadili sio sifa, hili suala limenitesa kwa muda refu, hadi ikafika pahala nikasema namuachia Mungu"

Katika ujumbe huo alimuomba msamaha mke wake na imani yake atamkubalia kama binadamu.

Kulingana na ujumbe wa pande hizo mbili, mashabiki wameonekana kuwa njia panda kujua ukweli wa suala hilo huku wengine wakimtaka Harmonize, kuanika ukweli kuhusu vipimo vya DNA ambavyo mke wake amevisema ili kuondoa shaka kuhusu baba wa mtoto huyo.

BASI SAWA

## Bumbuli anapolia 'Sina Wasi'

MSANII chipukizi wa kizazi kipya, Bumbuli, anatarajia kutoa ngoma yake mpya iitwayo 'Sina Wasi', akimshirikisha Beka Flavour.

Bumbuli ambaye hivi karibuni nyimbo zake zilitamba kwenye kampeni ya uchaguzi wa CCM, amesema kuwa ngoma hiyo anarekodiwa kwenye studio za Mafia, ameneo ya Barakuda, Tabata jijini Dar es Salaam.



Msanii huyo amesema ameingia studio baada ya kupata msaada kutoka kwa Mbunge wa Ilemela, Angelina Mabula.

"Yule mama ni mshauri wangu mkubwa, nimejifunza vingi kutoka kwake, hamchagui mtu wa kumsaidia. Amenisaidia sana na mpaka sasa amekuwa akinisaidia na kunipa ushauri, yeye ndiye aliniwezesha mpaka sasa ngoma hiyo inakaribia kutoka," amesema Bumbuli.

## H Baba kwa hili una Baraka zote

MSANII wa Bongo Fleva, H Baba, amempatia zawadi ya nyumba mama yake yenye thamani ya Sh.milioni 200.

Akizungumza na EATV, mwanamuziki huyo amesema nyumba hiyo ameijenga eneo la Nyasaka Jijini Mwanza.



"Mimi natokea kwenye familia ya kimaskini mama hakuwa na ile hali ya furaha kwa sababu nilikuwa sijawahi kumfanyia kitu kikubwa, nilichofanya ni kumjengea nyumba ya kwanza akapangisha ya pili akasema ipo mbali na Jiji hivyo hawezi kuishi peke yake ndiyo maana nikamjengea hii ya tatu" amesema H Baba



## Ben Pol heri yako kumtambua Barnaba

MWANAMUZIKI nyota wa R&B, Ben Pol, amemshushia sifa nyingi msanii mwenzake, Barnaba Classic, akisema ni nguzo katika kupandisha muziki wa Bongo Fleva.

Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram Ben Pol ameandika.

"Siku ya tatu leo nimekuwa nikifikiria jinsi ya kumuandika huyu mwamba, leo nimesema sitaki kupatia kuandika, nataka niandike hivyo hivyo ninavyojisikia kuhusu yeye, kwanza amefanya hit songs zisizopungua 300 za kwake mwenyewe, za kuandikia wengine na zile za kuchangia uandishi kwa watu"

Kisha akaendelea "Amewavutia wasanii wengi mno! hata kama wengine hawatasema leo, Mimi mwenyewe nishawahi kuwa namsindikiza, siku hizi wanaitwa Chawa, enzi hizo akienda studio kwa Allan Mapigo Masaki ili mradi tu awe ananifundisha maujanja yake ya kuimba na kutunga".

## Utata wa Shemeji: Shemeji Dar es Salam, mambo si salama

**Na Adam Fungamwango**

KUNA mambo mengine yanashangaza sana. Yaani mtu anatoka nyumbani kwake kwenda kuishi kwa mtu mwingine, kwa sababu tu ya kufikiria kule kuna malisho mazuri kuliko kwake.

Huko ni kutafutana lawama. Waswahili wanasema nyumbani ni nyumbani tu, iwe kubaya au kuzuri. Kuna hii filamu ya 'Utata wa Shemeji' inayoonyesha jinsi baadhi ya watu ambao wanafikiri kuwa mjini ni kila kitu. Yaani mtu akisikia Dar es Salaam, basi anaona kama vile ni sehemu ya raha tu. Kila kitu atakipata bure. Au maisha yake ni rahisi sana. Ukweli sivyo hivo. Dar es Salaam ni jiji lenye changamoto nyingi. Kila kitu ni pesa.

Filamu hii imechezwa na Burton Richard, Shukuru Hassan, Ally Kalawi, Neema Kalimba, Faudhia Hassan na wengineo.

Barton anachoka maisha ya shamba. Anaona kwake ni magumu licha ya kwamba ana nyumba na shamba. Anachofanya ni kuuza shamba na nyumba kijiji na akili yake ikamtuka kwenda mjini Dar es Salaam kwa dada yake.

Dada yake ameolewa jijini Dar na




mwanaume ambaye ni Mwenyekiti wa Mtaa fulani. Anafika Dar na kupokewa vizuri, lakini hasemi kama atarudi lini.

Kinachofanyika kwake ni kwamba akapewa lifti, lakini akataka kupiga na honi. Barton akawapanda kichwani dada yake na shemeji ya Kalawi.

Kalawi kila akimuuliza mkewe kaka yake ataondoka lini kwa sababu mambo ya mjini wamepanga chumba kimoja na sebule, kaka analala sebuleni si vizuri.

Kibaya zaidi ni kwamba Barton alikuwa hataki kufanya kazi yoyote ile, bali kukaa nyumbani tu.

Mke anaona kama vile mumewe ana roho mbaya hataki ndugu wawepo. Baada ya kuzoea shemeji sasa nyuma ikawa kama ya kwake.

Akakutana na wanawake wa mjini. Akawa anawaleta hadi nyumbani kwa shemeji yake. Kibaya zaidi akawa anawadanganya kuwa nyumba ile ni ya kwake.

Barton akawachosha shemeji ya dada yake. Akawa kama yeye ndiyo baba mwenye nyumba na wenzake ndiyo wamewekwa tu hapo.

Mwisho wa siku, baada ya shangingi lake kupata taarifa sahihi kuwa nyumba ile si ya kwake ni ya shemeji yake na amepanga, mwanamama huyo akaamua kuvunja uhusiano.

Shengingi hilo likamueleza Kalawi kuwa aliahidiwa kupangiwa chumba na Barton. Kalawi naye akamwambia mwanadada huyo kuwa pale alipo analala sebuleni, hana mbele wala nyuma.

Barton baada ya kuona mambo yake yapo hadharani hali ikaanza kuwa mbaya.

Akaanza kujiona mkosefu mbele ya shemeji yake na dada yake. Akawaita na kuwaomba msamaha. Ndipo alipowaeleza ukweli kuwa aliuza kila kitu shamba kwa kudhania kuwa atakuja mjini na kuwa na maisha mazuri, kama wanavyodanganyana vijijini.

Mwisho akaomba msamaha na nauli arudi kijijini. Shemeji na dada yake wakamsamehe, akampa nauli, na pesa za kununulia shamba lingine ili aanze tena maisha mapya huko kijijini.





## Wini hela ya kula watu 10 unanunua wigi

MWANAMUZIKI wa kike anayekuja kwa kasi, Wini Tz, amesema wasanii wa aina yake wanatumia gharama kubwa kuliko wanaume.

Wini Tz amesema msanii wa kike anatakiwa apendeze kila wakati na kama hana menejimenti ya kumuongoza inakuwa vigumu.

"Vitu ni vingi kwa msanii wa kike anatakiwa apendeze kila wakati ila mimi napendaga kuwa asili, kitu cha gharama ambacho niliwahi kununua ni nywele zangu za milioni 1.5," amesema.

## HIZI NDIZO NYIMBO 5 ZA SOKA KWENYE DANSI

**Na Adam Fungamwango**

KWA siku za karibuni nadhani mashabiki wa muziki wamezisikia nyimbo za kuhamasisha timu ya taifa, Taifa Stars, na kusifia klabu za Simba na Yanga zikiimbwa na wasanii mbalimbali, wakiwemo Tunda Man, Diamond Platinumz wengineo.

Hii haikuanza leo. Hata miaka ya nyuma, bendi za muziki wa dansi zilikuwa zikipiga nyimbo mbalimbali zinazohusu soka. Zipo zilizokuwa zikiisifia timu ya taifa, Taifa Stars. Kuna zingine zilikuwa zikisifia klabu kubwa na kongwe kabisa za Simba na Yanga. Lakini kuna bendi zilikuwa zinaimba kusifia timu za mikoa ambazo bendi hizo zipo na hasa zile zilizokuwa zikitwaa Kombe la Taifa kwenye mchuano ya Taifa Cup.

Ikumbukwe kuwa wakati huo kulikuwa na michuano ya soka ya mikoa ambayo ilikuwa na msisimko mkubwa sana.

Leo tunaziangalia baadhi ya nyimbo hizo ambazo zilipigwa na bendi za dansi.

**Hongera Simba (Baba Gaston)**

Baba Gaston Ilunga wa Ilunga, mkongomani aliyekuwa akipiga muziki nchini Kenya, alitunga kibao cha kuisifia Simba baada ya kutwaa Kombe la Afrika Mashariki na Kati kwa mara ya kwanza mwaka 1974 ambalo kwa sasa linaitwa Kombe la Kagame.

Katika kibao hicho aliwataja wachezaji kadhaa ambao walicheza michuano hiyo kama Athumani Mambosasa, Shaaba Baraza, Mohamed Kajole, Omari Chogo, Adam Sabu, Abdallaah Kibadeni na wengineo.

**Yanga Bingwa (Western Jazz)**

Yanga nayo ilitungiwa wimbo wa bendi maarufu ya Western Jazz baada ya kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 1968, hadi 1972.

Katika wimbo huo, wachezaji wanaoimbwa humo ni kila Abdurahman Juma, Adam Chipukizi, Baraka Kitenge (Baba yake mzazi mtangazaji Maulid Kitenge) na wengineo.

**Taifa Stars (Orchestra Safari Sound)**

Mwanzoni mwa miaka ya 1980, bendi ya Orchestra Safari Sound chini ya Fred Ndala Kasheba ilitoa kibao walichokiita 'Taifa Stars'. Ilikuwa ni baada ya wachezaji wa timu hiyo kutishia kujiuzulu baada ya kufungwa bao 1-0 na timu ya taifa ya Uganda.

Kibao hicho kiliwaasa wasijiuzulu na waendelee kulipambania taifa na kweli, timu ikaenda ugenini na kushinda mabao 3-1, mawili ya Zamoyoni Mogella na moja la Celestine 'Sikinde' Mbunga.

**Wanasoka (Mbaraka Mwinshehe)**

Mbaraka Mwinshehe na bendi ya Morogoro Jazz Band alitoa kibao kiitwacho 'Wanasoka' ambacho kilikuwa ni kuwapongeza wachezaji wa timu ya mkoa wa Morogoro ambacho kilitwaa Kombe la Taifa mwaka 1970.

Baadhi ya wachezaji waliotajwa humo ni Kapteni Jongo, Mnyepe, Sembuli, Manga, Rajab, Chogo, Shomari, Njenje, Sabu na wengineo.

**Taifa Cup Tanga-Atomic Jazz Band**

Bendi ya Atomic Jazz haikuwa nyuma. Nayo ilitoa kibao ikilipa kile cha Morogoro Jazz, baada ya timu ya mkoa wa Tanga kutwaa Kombe la Taifa mwaka 1973.

Wachezaji waliotajwa humo ni Hemed, Makunda, Salim, Mwabuda, Zimbwe, Mbwana, Sharrif na wengineo waliolitwaa kombe hilo.





## Peter pole ya maneno haitoshi

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Peter Okoye, amemuelezea mwanasoka wa zamani kutoka nchini humo, Osazee Odemwingie, kwamba hayuko sawa na anahitaji msaada.

Mwimbaji huyo wa kundi la Psquare ambalo limevunjika, amesema hayo wakati akishiriki mazungumzo ya moja kwa moja katika ukurasa wake wa Istagram.

"Bro nilijaribu kupuuza lakini nimevunjika moyo sana, kama sasa uko karibu na Mungu haikufanyi uhisi wengine wako karibu na shetani. Ninavyokuona unaumwa na unahitaji msaada kwetu," amesema Peter.



## Eti! Burna Boy kumbe una kibinti pembeni?

STAA wa muziki kutoka Nigeria, Burna Boy, ameshutumiwa kwa kumtapeli mpenzi wake, Stefflon Don, kwa kujihusisha kimapenzi na msichana wa miaka 23, Jo Peal.

Peal amedai uhusiano wake na mwanamuziki huyo umekuwa wa siri na umedumu kwa kipindi cha miaka miwili sasa.

Burna Boy yuko kwenye mahaba mazito ma rapa Stefflon Don (28), raia wa Uingereza ambaye tayari wamechumbiana tangu mwaka 2019.


## Rihanna penzi jipya tena

SASA imethibitika kuwa mwanamuziki wa Marekani, Rihanna na rafiki wake wa siku nyingi, A$AP Rocky, wana uhusiano wa kimapenzi.

Kulingana na mtandao wa PageSix, imeeleza kuwa wawili hao ambao wote wana miaka 32, wamejulikana kama wapenzi baada ya kwenda kula chakula cha usiku katika hoteli ya Beatrice Inn, iliyoko New York.

Fununu za Rihanna kutoka kimapenzi na rafiki yake huyo zilianza miaka mitatu iliyopita baada ya kuachana na bilionea Hassan Jameel.





## Ikechukwu ukapera haulipi

RAPA wa Nigeria, Ikechukwu, ameanza safari ya kuuacha ukapera baada ya kumchumbia mpenzi wake wa siku nyingi.

Ikechukwu amemvisha pete ya uchumba mpenzi wake huyo na video yake aliisambaza katika mitandao ya kijamii.

Kwenye video huyo, anaonekana Ikechukwu akimuuliza mchumba wake kama yupo tayari kuwa mke wake, huku mwanamke hiyo akiitikia "Ndiyo".

## Lil Frosh sijui kama utavuka salama 2020

MWANAMITINDO ambaye ni mpenzi wa rapa, Lil Frosh, amedai alitishiwa kuuawa wakati akiishi pamoja na mwanamuziki huyo.

Iyomaterire Okeoghene Taiwo, alitoboa siri hiyo wakati akizungumza katika kipindi cha Televisheni kinachoongozwa naDaddy Freeze.

"Alinipiga vibaya sana, hapo ndipo aliponivua nguo na alikuwa kama anatuma kwenye mitandao ya kijamii, aliniambia nitaharibu maisha yako. Alinimwagia maji, akanipiga kofi, "amesema.



MAKALA

Na Mwandishi Wetu

# MWISHO MAPIGANO TIGRAY?

## ■Mekelle mikononi mwa vikosi vya serikali
## ■Waasi wakimbilia milimani, waapa kupigana



Wanamgambo wa TPLF wakionekana kabla ya kukimbia mji.

HATIMAYE Mji mkuu wa jimbo la Tigray, Mekelle, umeingia mikononi mwa vikosi vya jeshi la serikali ya Ethiopia, baada ya mapigano ya wiki kadhaa.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, ametangaza majeshi yake kuukamata mji huo na kuudhibiti kutoka mikononi mwa chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF), ambacho kilikuwa kikiongoza jimbo hilo kwa muda mrefu.

Katika taarifa yake, Abiy amesema katika kuukomboa mji huo kutoka kwa waasi, vikosi vya shirikisho vilizingatia usalama wa hali ya juu kwa wakazi wake nusu milioni.

Mapigano ya siku mbili yaliyojumuisha makombora ya ardhini na yale yanayotoka kwenye ndege za kivita, yalitosha kuwalegeza wanamgambo ta TPLF na kisha kuukimbia mji huo na kuelekea milimani.

Waziri mkuu huyo amesema ushindi huo waliutarajia kutokana na wanajeshi wake kuwa na mbinu na uimara wa kupigana.

**HOSPITALI YAELEMEWA**

Baada ya mji mkuu wa jimbo hilo la Tigray, kushambuliwa kwa makombora siku mbili mfululizo, athari zimeanza kuonekana baada ya kuwapo kwa taarifa kuhusu hospitali kuu ya jimbo hilo kuzidiwa na wagonjwa.

Imeelezwa hospitali hiyo inakabiliwa na uhaba wa vifaa baada ya mamia ya watu waliojeruhiwa kufikishwa hapo kwa ajili ya matibabu.

Hata hivyo taarifa chache ndizo zilizotoka katika kipindi chote cha mapigano kwa sababu ya kukatwa kwa mawasiliano.

Taarifa kutoka katika Shirika la kimataifa la msalaba mwekundu (ICRC), zinatoa mwanga kuhusu matukio yanayotokea wakati mzozo huo ukiendelea.

ICRC inasema magari ya wagonjwa ya Shirika la msalaba mwekundu la Ethiopia, yalifanya kazi ya ziada ya kuwabeba majeruhi walioumia na watu waliokufa kwenda katika hospitali ya rufaa Ayder.

Hata hivyo hospitali hiyo ilikuwa na asilimia 80 ya wagonjwa wenye majeraha makubwa yaliyosababishwa na mapigano hayo.

"Hospitali zinakabiliwa na hatari ya uhaba wa vifaa pamoja na dawa kama vile za kuua bakteria, za maumivu na glovu ," anasema mkuu wa ICRC nchini Ethiopia, Maria Soledad.

Hospitali hiyo pia imeishiwa na mifuko ya kuhifadhia miili ya watu walipoteza maisha na kuwepo na uhaba wa vyumba vya kuhifadhi.

ICRC, hatahivyo, haikutoa takwimu zozote za idadi ya watu walioumia au kufa katika mapigano hayo.

**SERIKALI YAHITIMISHA**

Katika taarifa iliyotumwa kwenye mtandao wa Twitter Jumamosi ya wiki iliyopita, Waziri Mkuu wa nchi hiyo, alisema jeshi limechukua udhibiti kamili wa Mekelle na kwa hali hiyo inahitimisha awamu ya mwisho ya jeshi.

"Ninafurahi kuwashirikisha kwamba tumekamilisha na tumesitisha harakati za kijeshi katika jimbo la Tigray," alisema Abiy.

Akaongeza kwa kusema kuwa jeshi liliwaachilia maelfu ya wanajeshi waliokuwa wametekwa na TPLF na linadhibiti uwanja wa ndege na ofisi za jimbo.

Kiongozi huyo amekuwa akiuelezea mara kwa mara uongozi wa TPLF kama kikundi cha uhalifu na kwamba viongozi wake watapelekwa mahakamani.

**TPLF: TUTAENDELEA KUPIGANA**

Katika ujumbe wake wa simu kwa shirika la habari la Reuters, kiongozi wa TPLF, Debretsion Gebremichael, licha ya kutozungumzia moja kwa moja kushindwa kwa kikosi chake, anasema ukatili wao unaweza kuonekana katika mapambano yao dhidi ya wavamizi.

"Tutaendelea kupigana, hii inahusu kulinda haki yetu ya kujiamlia mambo yetu ." anasema Gebremichael.

Hata hivyo, haijajulikana sehemu aliko kiongozi huyo.

Katika taarifa hiyo iliyosomwa katika televisheni ya jimbo la Tigray, ilisema "Mashambulio ya mabomu ya Mafashisti yamesababisha vifo vya raia na majeruhi. Serikali ya Tigray imeapa itachukua hatua za kujibu dhidi ya mashambulio ya mabomu ".

Baadhi ya wachambuzi wanasema TPLF wanaweza kukimbilia maeneo ya milimani, huko wanajiandaa kuanzisha mashambulio mengine ya kuvizia dhidi ya vikosi vya serikali ya shirikisho.

**NGUMU KUFIKA**

Hivi karibuni serikali ilikubali kuwaruhusu watoa misaada wa Umoja wa Mataifa, kuingia Mekelle kwa ajili ya kugawa vyakula na misaada mingine.

Lakini umoja huo, umeonya kuhusu uwezekano wa kutokea kwa uhalifu wa kivita.

Pia ulikuwa umeelezea wasiwasi wake kuhusu kutokuwa na uwezekano wa wahudumu wa misaada ya kiutu kuyafikia maeneo yaliyoathika.

Vikosi vya Ethiopia vilipelekwa katika mpaka baina Tigray na Sudan, kuwazuia watu kuikimbia nchi. Katika tripoti ya Umoja wa Mataifa, inaeleza zaidi ya Waethiopia 40,000 walikuwa wamevuka mpaka tangu mgogoro huo ulipoanza mapema mwezi wa Novemba.

**TPLF NI NANI?**

Wapiganaji wa TPLF, wanatoka katika kikosi cha kijeshi pamoja na wanamgambo waliopata mafunzo mazuri kutoka eneo hilo, wanakadiriwa kufikia 250,000.

TPLF ilianzishwa miaka ya 1970 na kuongoza harakati zao dhidi ya utawala wa dikteta aliyekuwa na itikadi za kijamaa, Mengistu Haile Mariam, ambaye alipinduliwa mwaka 1991.

Kikundi hicho kiligeuka kuwa na ushawishi wa kisiasa katika nchi iyo, hadi alipoingia madarakani Abiy Ahmed mwaka 2018.TY IMAGES

Mgogoro huo ilikuwa wa muda mrefu na kuchochea uhasama kati ya serikali ya Ethiopia na chama cha TPLF.

Wakati Abiy alipoahirisha uchaguzi mkuu kwa sababu ya ugonjwa wa Covid-19, uhusiano ulizidi kuzorota baada ya TPLF, kuendelea na uchaguzi wao katika jimbo la Tigray.

TPLF ilisema kuwa muda wa serikali wa kuongoza taifa hilo umeisha, ikidai Abiy hana uwezo wa kimamlaka.

Mapema mwezi wa Novemba, wapiganaji wa TPLF waliingia katika ngome ya jeshi katika mji wa Mekelle na kuteka silaha na kujeruhi baadhi ya wanajeshi.

**Kwa msaada wa BBC**



# Simulizi za kijinsia zinavyosaidia wanawake kujua haki zao

**Na Mwandishi Wetu**

PROGRAMU ya Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP) imekuwa ikiendesha vituo simulizi ili kuongeza uelewa juu ya maswala yanayohusiana na jinsia ili kufikia usawa katika muundo wa jamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, anasema kuwa vituo maarufu vya kusimulia hadithi, maarufu kwa kiswahili kama 'vilinge' vina mbinu zinazowezesha mazungumzo na majadiliano kama kazi ya vikundi, tafiti, vikundi vya kijiweni, kujadiliana na kutazama video kwa pamoja.

Lengo kuu ni kuhakikisha kuwa maisha ya wanawake na vikundi vingine vilivyo katika mazingira magumu katika jamii yanaboreka na unyanyasaji dhidi yao unapigwa vita vikali.

Baadhi ya mikoa ambayo imenufaika na vituo hivi vya kusimulia hadithi ni Kilimanjaro, Mbeya na Pwani, ambapo viongozi wa wanawake wamepongeza mikutano hiyo, ambayo imefungua kurasa mpya za kihistoria katika maisha yao.

Hadija Said Mwanahomboza kutoka eneo la Masaki, Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani anakubali kwamba "vilinge" vimemsaidia kufahamu kuhusu ukatili wa kijinsia katika eneo lake.

Mwanamke huyu wa makamo sasa ana uwezo wa kuelezea aina tofauti za Ukatili wa kijinsia, Haki za Binadamu katika muktadha wa haki, na pia anaweza kuandaa mpango wa hatua juu ya jinsi ya kudhibiti unyanyasaji kwa wanawake na vikundi vingine vilivyo katika eneo lake.

"Nimejifunza aina tofauti za unyanyasaji wa kijinsia nyumbani, mahali pa kazi na katika maswala ya jamii ya jinsia na haki za binadamu, mipango ya utekelezaji na mabadiliko.

Wakati wa mkutano kwa njia ya simu uliofanyika makao makuu ya TGNP huko Mabibo, Dar es Salaam hivi karibuni, Deogratias Temba, mkufunzi wa jinsia alisema kuwa TGNP kawaida huendesha vituo vya kusimulia hadithi ili kuwapa wanawake fursa ya kusimulia mafanikio yao na changamoto za maendeleo ambazo ziko katika maeneo yao ya makazi. .

"Tunavutiwa zaidi na ujenzi wa uwezo, kuhakikisha kuwa wanawake tunaowafundisha wanapata uwezo wa kushughulikia changamoto za jinsia na maendeleo wanazokabiliana nazo katika maisha yao ya kila siku. Tunawafundisha pia jinsi ya kuboresha maisha yao kwa kujiunga na vituo vya mikopo katika vijiji vyao. "anasema Temba.

Lakini, mwanzilishi wa vikoba ni nani? Ni Devota Likokola, mwanasiasa mashuhuri ambaye pia amehudumu kama mbunge kwa miaka kumi.



Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, akizungumza katika moja ya kongamano la utetezi wa jinsia.

Devota Likokola ambaye pia alishiriki mahojiano hayo na wanawake ambao wamefaidika na TGNP 'vilinge' anasema kwa nguvu kwamba wakati wanawake wamefundishwa vizuri, wanaweza kupata mapato mazuri, sio kwao tu, bali kwa jamii kwa ujumla.

Leo, neno 'Vicoba' linajulikana kila kona ya nchi na vikundi vya wanawake na vijana vimejiunga nao katika maeneo yao, kama fursa ya kukusanya mtaji kwa njia ya mikopo, ili wahusika waweze kuongeza mapato yao.

Alisimulia historia yake ya kibinafsi, kwamba alifanya kazi benki ya NBC na aliacha kazi mnamo 1989, na aliamua kufungua mgahawa wa kibinafsi kama uwekezaji wake, kabla ya kuhamia zaidi katika uwanja wa kisiasa.

"Nilipoacha kazi nilifungua mgahawa, hata hivyo niliingia kwenye siasa na kuwa diwani wa Songea na baadaye nikaingia bungeni," anasema.

Devota anaongeza kuwa katika kipindi hicho, aliamua kuanzisha kituo endelevu cha mikopo inayolenga kuwakomboa wanawake kimaendeleo.

Leo anajivunia kuwa mpango huo umesaidia wanawake wengi kujiongezea kipato, ambacho kimekuwa msaada mkubwa katika kukidhi mahitaji ya watoto wao kama vile kuwapeleka shule nzuri, na pia kujijengea nyumba nzuri.

Likokola ambaye alishiriki kwenye mahojiano hayo kwa njia ya simu na wanawake ambao wamefaidika na TGNP 'vilinge' anasema kwa nguvu kwamba wakati wanawake wamefundishwa vizuri, wanaweza kupata mapato mazuri, sio kwao tu, bali kwa jamii kwa ujumla.

Devota ambaye alitumia mkutano huo kuwafundisha wanawake jinsi ya kubadilisha maisha yao kuwa bora, anasema kuwa wanawake wengi wanakabiliwa na changamoto kubwa katika maendeleo yao ya kibinafsi kwa sababu hawajapewa maarifa sahihi ya kufanya kazi kwa bidii katika kuboresha maisha yao ya kijamii na kiuchumi.

Lengo ni kusimamia vikundi vidogo vya wanachama ambao wamefundishwa. Serikali pia imekuwa ikihimiza watu kuja katika mabaraza mbali mbali ili kujiunga na vikundi kama hivyo, ili walengwa waweze kufaidika "Anasema.

Juliet Mkonyi ambaye ni Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kati cha Kibosho anasema amenufaika na vipindi vya TGNP, na sasa ameweza kujenga mabweni katika shule zingine za kata, na pia kuboresha utoaji wa huduma katika zahanati zingine zilizo katika eneo lake.

"Baada ya kusikia kile Mama Devota Likokola alisema juu ya kuboresha maisha ya wanawake, sasa ninaweza kuweka mipango ya jinsi ya kuwapa vifaa vya mikopo kwa wanawake kuwawezesha kuendesha businesse ndogo ndani nje ya kijiji chetu" anasema.

Paulina Shirima ambaye anafanya kazi katika kijiji cha Okaoni akibainisha kile mwenzake Mkonyi anasema, akiongeza kuwa amejitahidi kusaidia wanawake kuanza kilimo cha horticluture huko Umbwe Okaoni, ambapo wamefanikiwa kutoa aina tofauti za mboga za majani ikiwamo na, saladi, nyanya na cabage.

Anaelezea changamoto alizokabiliwa nazo kama ukosefu wa usafiri wa uhakika wa kuwatembelea wanawake nyumbani kwao kutathmini kazi zao. Wanawake wachache aliofanikiwa kuwatembelea waliwapata wamefanikiwa sana.

Mwanaisha Waziri anayeishi katika mkoa wa Pwani ni wanawake wengine ambao wamefaidika na kituo cha kusimulia hadithi cha TGNP, ambaye anasema kwa nguvu kwamba katika kijiji chake hakukuwa na shule ya sekondari lakini wamefanikiwa kujenga moja, na hadi sasa wamewejenga vyumba vitatu vya madarasa, walimu ofisi, na choo cha shimo.

"Tuna kamati za wazazi wenye nguvu ambazo hukutana mara nyingi kuhakikisha kuwa watu wanachangia pesa kuwezesha ujenzi wa shule hii. Mafunzo ya TGNP yamesaidia viongozi wa wanawake kujua majukumu yao katika jamii, na sasa wana ujasiri wa kuzungumza bila woga "anasema Mwanaisha.

Sharifa Issa Salum kutoka Kata ya Kibuta wilayani Kisarawe anasema kwa kujigamba kuwa kwa kushirikiana na wanaume katika eneo lake, wanawake wameweza kuchimba kisima cha maji ambacho kimetatua shida ya maji katika kijiji hicho na watoto zaidi wameanza kwenda shule, shukrani kwa mafunzo ya TGNP ambazo zimehamasisha wanawake juu ya majukumu yao katika jamii.

TGNP inafahamu kuwa bila ujumuishaji wa wanawake kwenye shughuli za kiuchumi hakuna chochote endelevu katika kufanikisha maendeleo kinaweza kutekelezwa.

TGNP inaendesha semina nchi nzima kuwawezesha wanawake katika vituo vyao vya maarifa vilivyowekwa ili kuwawezesha kama kikundi kuwa endelevu na kila mshiriki mmoja katika vituo hivi kuwa na uwezo wa kiuchumi.

Miongoni mwa mipango mingi ni utekelezaji wa Miradi ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi (WEE) ambayo ililenga kuwezesha jamii ya msingi kuanzisha na kuendesha vituo bora vya Maarifa ambavyo vinasaidia wanachama kuanza na kuendesha shughuli za kuongeza mapato katika jamii za vijijini kama Wilaya za Kisarawe, Moshi Vijijini na Morogoro. .

Kuwawezesha wanawake wenye ujuzi na ujuzi wa mjasiriamali huwaangazia kujua jinsi ya kushughulikia changamoto zinazowakabili katika shughuli zao za kiuchumi za kila siku.

TGNP inafanya kazi na wadau wanaotetea haki za wanawake kumaliza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake na vikundi vingine vilivyotengwa, iwe kwa sababu ya darasa, jinsia, umri na ulemavu.

Uwezeshaji wanawake lazima uanzie chini, ambapo wengi wao hawana sauti ya kijamii na kiuchumi na kisiasa.

Mdau yeyote, liwe shirika la kike linalojitahidi kuchangia kujenga harakati mahiri ya mabadiliko ya kike ya kukuza usawa wa kijinsia na usawa, uwezeshaji wa wanawake na haki ya kijamii ni mshirika wa TGNP katika biashara.

Ikiwa wanawake watawezeshwa kiuchumi, kuna uwezekano mkubwa kwamba watoto wao wataenda shule, kupata afya bora na kuvaa vizuri na zaidi ya yote familia nzima itakuwa imara na kuhakikishiwa chakula cha mraba kila siku.

## HABARI KIMATAIFA

# Kenyatta awanyooshea kidole wafadhili

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ameapa kutotoa nafasi kwa nchi za nje kujaribu kuingilia na kuelekeza serikali yake nini wafanye kwa raia wa nchi hiyo.

Kiongozi huyo, alisema hayo wakati akifungua kongamano la magavana ambalo litajadili mikakati ya kuboresha uchumi jijini Nairobi.

Rais Kenyatta, alizishukuru baadhi ya nchi kwa kumuunga mkono na kumpa ushirikiano, lakini alisisitiza hatakubali kulazimishwa nini afanye na mtu yeyote.

**Tunakuomba ujiunge nasi, utuunge mkono katika juhudi zetu hizo. Lakini usiingilie kwasababu hatutakuruhusu uamuru njia tunayostahili kufuata.**

"Tunashuku maofisa wa Umoja wa Mataifa na washirika wengine wa maendeleo ambao wamekuwa karibu sana lakini hadi kufikia sasa lazima niweke wazi, wakati tunawashukuru kwa ushirikiano wenu na kutajarajia ushirikiano zaidi, lazima mkumbuke Kenya ina wenyewe na wenyewe ni Wakenya milioni 50," alisema Kenyatta.

Aidha, Kenyatta aliwaomba kujizuia kujaribu kuwaelekeza kitu cha kufanya na njia za kufuata.

"Tunakoelekea kuko wazi. Tunakuomba ujiunge nasi, utuunge mkono katika juhudi zetu hizo. Lakini usiingilie kwasababu hatutakuruhusu uamuru njia tunayostahili kufuata. Nawaomba kwa heshima kubwa mtuheshimu ndio tuwaheshimu. Kila mtu ana shida zake hata kama wana shida wanazohitaji kuzitatua huko kwao. Nasema hivyo kwa nia njema tu. Sitaruhusu hilo na kama nchi hatutaruhusu hilo." Alisistiza.

Wakati huo huo, mwisho wa Gavana wa Nairobi, Mike Sonko, umetimia baada ya madiwani kupiga kura ya kutokuwa na imani naye.

Katika upigaji wa kura hizo, madiwani 88 kati ya 122 wa wa kaunti ya Nairobi, walipiga kura ya kutokuwa na imani na kiongozi hiyo, idadi ambayo imefika kiwango cha theluthi tatu zinazotakiwa kumuondoa madarakani.

Baada ya hatua hiyo kukamilika, matokeo hayo yatawasilishwa mbele ya bunge la Seneti ambao watajadili na kutoa uamuzi wa mwisho kuhusu hatima ya gavana hiyo.

Awali, gavana huyo aliwasilisha maombi katika mahakama kuu kuomba kusitisha kikao hicho cha kumuondoa madarakani, akieleza ni kitendo hicho ni kinyume cha sheria na katiba ya Kenya.

Gavana Sonko ambaye kipindi fulani alikuwa na nguvu na ushawishi wa aina yake katika kaunti hiyo na kumfanya kuongoza kwa vipindi viwili mfululiozo.

Endapo bunge la seneti litakubaliana na matokeo ya kura ya kutokuwa na imani naye iliyopigwa na madiwani, hapo ndipo itakuwa mwisho wa utawala wake na kuandaliwa kwa uchaguzi mpya katika kaunti hiyo wa kumchagua gavana na naibu wapya.

Hata hivyo, hadi anapigiwa kura hiyo, Sonko alikuwa hana naibu gavana. **BBC**

# Biden kuwaomba raia kuvaa barakoa siku 100

**WASHINGTON,** Marekani


RAIS mteule wa Marekani, Joe Biden, amesema anapanga kutoa agizo litakalowalazimu raia wa taifa hilo kuvaa barakoa katika majengo ya serikali na vituo vya kusafiri kwa siku 100 za kwanza za utawala wake.

Biden alisema kwenye mahojiano na kituo cha utangazaji cha CNN, kuwa atawaomba raia kuvaa barakoa kwa siku hizo na si muda wote, na anaamini watashuhudia kupungua kwa kiasi kikubwa maambukizi mapya.

Baada ya likizo ya sikukuu ya shukrani wiki iliyopita, kumeongezeka maambukizi mapya na vifo vitokanavyo na virusi vya corona.

Kwa juzi pekee kuliripotiwa zaidi ya visa vipya 210,000 na vifo 2,907.

Aidha, kwenye mahojiano hayo. Biden alisema atapendelea Mtaalamu Mwandamizi wa Magonjwa ya Kuambukiza Dk. Anthony Fauci, kubakia kuwa mkuu wa taasisi ya kitaifa ya magonjwa ya kuambikiza na ya mzio. **DW**





Wakimbizi wa Rohingya watahamishwa katika kisiwa cha a Bhasan Char, pichani baadhi wakiwa katika mabasi maalum kwa ajili ya kutoka kwenye kambi yao ya sasa ya Chattogram, nchini Bangladesh. **PICHA: REUTERS**

# Umoja wa Ulaya yaitaka Ethiopia kufungua mawasiliano Tigray

**KHARTUM,** Sudan

KAMISHNA wa Umoja wa Ulaya kuhusu usimamizi wa migogoro, ameitaka serikali ya Ethiopia kurudisha mawasiliano katika jimbo la Tigray.

Hata hivyo, ilihimiza pande zote zinazopambana katika jimbo hilo kusitisha mapigano.

Kiongozi huyo, Janez Lenarcic, yuko nchini Sudan ambako alikwenda kutazama hali ya wakimbizi wanaokimbia mapigano nchini mwao.

Akizungumza kutoka kambi ya Um Raquba, juzi ambako alikutana na wakimbizi hao na kuzungumza nao, alitoa wito kwa serikali ya shirikisho kufungua njia za mawasiliano iliyoyafunga katika jimbo la Tigray.

Kamishna huyo alieleza kwamba amezungumza na wakimbizi kadhaa kwenye kambi hiyo, kinachomsikitisha ni kusikia wengi wao hawana taarifa yoyote kuhusu ndugu, jamaa zao na marafiki zao waliowaacha Tigray.

"Unajua hata bado hatujafika, misafara iliyokuwa ikipeleka msaada kwenye eneo hilo kabla ya kuanza vita ilisimama baada ya operesheni ya kijeshi na mpaka sasa bado haijaweza kuondoka. Hiyo ndiyo hali iliyopo". Alisema.

Aliongeza "Kuhusu msaada mpya wa kibinadamu ambao utayaangalia mahitaji mapya yaliyojitokeza kutokana na vita hivi, ni lazima kwanza tutathmini kinachohitajika".

Ethiopia ilitangaza siku ya Jumatano ya wiki hii, kufungua njia ili kuruhusu Umoja wa Mataifa kupeleka msaada Tigray kwa mujibu wa shirika la habari la AFP.

Kwenye makubaliano hayo, ilielezwa wazi kwamba Umoja wa Mataifa na washirika wake wa masuala ya kiutu wanaweza kuwapelekea msaada raia kwenye maeneo yanayodhibitiwa na serikali ndani ya jimbo hilo hilo.

Hatua hiyo ililalamikiwa na Umoja huo kuwa vita inayoendelea inazuia juhudi za kupeleka msaada.

Lakini pia upande mwingine taarifa zilizotoka kwa wanajeshi wa Sudan, ambao walikataa kutajwa majina yao, zilisema wanajeshi wa serikali kuu ya Ethiopia juzi waliwazuia watu waliokuwa wakilikimbia jimbo la Tigray kuvuka mpaka kuingia upande wa pili.

Matukio hayo yanafuatia madai mengine kama hayo yaliyotolewa na wakimbizi siku kadhaa za nyuma wakieleza kwamba wanajeshi hao waliwasimamisha na kuwazuia kuondoka jimboni humo.

Wanajeshi wa Sudan walisema waliweka usalama kwenye eneo hilo na baadaye juzi jioni mpaka huo ulifungwa, pia waandishi habari wa shirika la habari la Associated Press walisema waliona watu kadhaa wakiwa wanasubiri kuvuka katika eneo hilo la mpaka upande wa Ethiopia. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**

## NAFASI ZA KAZI

**Nafasi za kazi ya ualimu Diploma**
**- Kiswahili**
**-Science SST**
**- Kiingereza**
**Mawasiliano:**
**0783 334653**


NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA VYETI



**DYNESS ELIASAFU MSIGWA** anatangaza kupotelewa kwa vyeti cha kidato cha nne chenye index namba **S1163-0026** kilichotolewa na baraza la mitithani kupitia shule ya secondary UJENZI mwaka 2013 na cheti cha chuo DIPLOMA registration namba **NS1163/0026/2013** chuo cha **KILIMANJARO SCHOOL OF PHARMACY** mwaka 2019,yeyote atakayeviokota atoe taarifa
**Polisi taarifa KIL/MOS/RB/667987/2020**
**Mawasiliano 0746443196**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WATOTO IRINGA**
**IRINGA**

**SHAURI LA MADAI NO: 22/2020**

**HAMISI KULWA ALLY..........................MDAI**
**DHIDI YA**
**MARRY PRISCO MLAMBYA ............MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

Shauri tajwa hapo juu limepangwa kutajwa tarehe 11/12/2020 saa mbili na nusu (8:30) asubuhi hivyo mjibu maombi katika shauri hilo unatakiwa kufika katika Mahakama ya watoto Iringa ama umtume mwakilishi wako.

Fahamu kuwa endapo kama hautafika siku hiyo au kutuma mwakilishi wako, shauri hilo litapangwa tarehe ya kusikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Anuani ya simu:ARDHI
Simu: 2548570 au 2502805
Telefax 23244
Telex 2271

Baraza la Ardhi na Nyumba,
S.L.P 5058,
TANGA.

**Unapojibu tafadhali taja:** **1/12/2020**

**Kumb Na.Appl.No.67/2016**

**YAH:** SHAURI NA 86 LA 2019

**THE REGISTERED TRUSTEES OF NORTH EASTERN DIOCESE OF EVANGLICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA.......................................**MDAI
DHIDI
RAMADHANI OMARI KIDIZI
MASHAKA SHUGA ............................................................WADAIWA

**KWA: MASHAKA SHUGA-POPOTE ULIPO**

Mwombaji alietajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako katika Baraza la Ardhi Nyumba Wilaya ya Tanga

Unaarifiwa kufika mnamo tarehe 17/12/2020 saa tano (5:00) asubuhi ambapo shauri hili litakuja kutajwa. Hivyo basi unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga.

Endapo hutatekeleza haya, shauri hili litasikilizwa upande mmoja mmoja na Hukumu kutolewa dhidi yako.

**AMRI.** Hii imetolewa kwa mkono wangu na mhuri/lakiri ya Baraza hili leo tarehe 1/12/2020.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**TANGA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO.**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI/TARAKA/MIRATHI;NAMBA:330..2020**
**Mdai: .......................................JOHN WAZIRI**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa:................. JOHN SEVELIN@MGONA**
**Kwa JOHN SEVELIN@MGONA WA MBEZI DAR ES SALAAM.**
**Ombi la Mdai: .......................JOHN WAZIRI**
**Madai ya: ...........................PESA SH. 4,400,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 07 mwezi 12 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi/alasiri.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 26 mwezi 11 mwaka 2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

116028702

## KUPOTEA KWA CHETI



**RICHARD ALLY MPANDUZI** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0729-0089** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MSOLWA mwaka 2011,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/CHA/RB/825798/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**VICTOR LAZARO SWAI**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili
**MC 846 CBZ**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi
Taarifa ya Polisi
**ARU/ARU/RB/561681/2020**

116029302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;342/2020**

**Ombi la MASHAKA ATHUMANI KIMANGA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ATHUMANI SAID KIMANGA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 15/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 13/11/2020.

116028902

## CHETI KIMEPOTEA



**LAURENT JIGALU IPINDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye No. **S.1460/0021** kilichotolewa na shule ya secondary MWANHALA mwaka 2016. yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.taarifa ya polisi: **NUN/RB/1296/2019.**


NJOO UTANGAZE
BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini-**41**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

NGUMI ilirushwa ambayo ilikusudiwa kutua kwenye taya. Hii aliikwepa. Tayari adui alitambua kuwa mpinzani wake ameangusha bastola, hivyo asingeweza kumfanya lolote. Alikosema. Eddy aliikwepa kwa ustadi iliyomshangaza mtu huyo. Wakati akishangaa, Eddy alirusha mateke mawili yaliyokwenda sawia kwenye kwenye kifua cha jamaa yule.

Hapo ndipo alipogundua kuwa hakuwa mbele ya mtu wa kawaida. Ni mjuzi hasa. Akaamua kubadilisha mipigo. Aliachia teke la kuzunguka, ambalo limpata Eddy kwenye mbavu. Alijifanya ameumia sana.

Hakujua kuwa alidanganywa. Eddy ni mpelelezi maarufu nchini Tanzania ambaye amefundishwa vitu vingi vya kikomandoo, hivyo teke lile lisingemtoa kwenye reli.

Aliendа mzima mzima kwa lengo la kutaka kummaliza, baada ya kuona amemlegeza. Alikiona cha moto. Eddy alipeleka mapigo matatu ya karate mbili za kifua na moja ya tumbo, ikamrusha hatua kadhaa nyuma na kuanza kutapika damu.

Tukio lile lilimuogopesha sana mwenzake na kumfanya atetemeke mwili mzima. "Hallo hallo Makao Makuu. Naomba mje na kikosi hapa, kuna kikundi cha wahalifu hapa kilituvamia. Sijajua nia yao, lakini hayo mengine tutayajua ofisini, naomba askari na gari la wagonjwa, pamoja na la kukokota magari mabovu" alipiga simu ofisini kwake.

Saa yake ilimuonyesha imetimua saa tatu usiku. Magari yaliwasili na kuwachukua wote. Yeye hakuondoka.

Alirejea kwenye makaburi alipozikwa Patiyo na Grace. Alimkuta Shani akiwa amelala kifudifudi kama alivyoambiwa. Lakini akiwa anatetemeka kwa hofu.

"Yameisha mpenzi. Tumepona, sasa tunaweza kwenda nyumbani."

"Nimesikia milio ya risasi nikajua wameshakuua mpenzi wangu, niliogopa sana."

"Wasingeweza kumuua mlinzi wa Shani."

"Kwani walitaka kumuua nani?"

"Wote sisi wawili."

****************************

Ni wiki moja imepita tangu tukio hilo kutokea. Eddy alikuwa amewaagiza watu wa idara yake kuwashughulikia watu hao ili waseme ni nani alikuwa amewatuma.




**Kwa jinsi sakata zima alivyolifuatilia, aligundua kuwa inawezekana Jim akawa amewakodi watu walewale ambao walimuua mdogo wake Patiyo bila yeye kujua ili wamuue Shani.**

Kazi ilifanyika ingawa si kirahisi kama walivyotarajia. Walionekana kuwa ni wahalifu waliokubuhu.

Akiwa kwenye kiti chake cha kuzunguka alionekana kama mmoja wa maafisa kijana.

Alikuwa tofauti na yule wa wiki moja iliyopita. Yule aliyekuwa akipigana na maharamia maeneo ya Kinondoni Mwembejini Makaburini jijini Dar es Salaam. Yule aliyewashangaza walioтumwa kazi hiyo ambayo ilionekana kuwa nyepesi kama kuua mbu, lakini ikawa nzito kama kubeba gunia la misumari na kulivusha ng'ambo ya bahari.

Mlango wa ofisi wake ulifunguliwa. Aliyeingia ni mmoja wa wasaidizi wake.

Amour alikaa kwa heshema pkwenye kiti kinachoangalia na bosi wake.

Mkononi alikuwa ameshika karatasi mbili. Alitazama usoni bosi wake na akaanza kueleza.

"Bosi nimekuletea taarifa, baada ya kazi kufanyika kwa wale wahalifu." Alisema na kuondoa macho yake kumtazama bosi wake, yakaelekea kwenye karatasi.

"Baada ya kuwatingisha, kuna mambo tumeyafahamu. Nimekuja kukupa mrejesho.

Wa kwanza anaitwa Tamim Hussein. Huyu jamaa anaonekana ndiye hatari zaidi kuliko wenzake. Ni mtaalam wa shabaha. Huyu ni jambazi hatari sana. Ndiye anayetumiwa kulennga shabaha. Bosi tumegundua kuwa ameshiriki matukio mengi sana. Hata lile la kumuua Patiyo na mkewe Grace, yeye ndiye aliyefanya kazi hiyo." Alisema Amour na kumuona bosi wake akikunja sura.

Hiyo ilimshtua Eddy. Lakini pia ilimpa faraja. Siku zote alikuwa akipiganía suala ya mpenzi wake Shani limalizike, ili aanze kuchunguza juu ya kifo cha shangazi yake Grace na mumewe Patiyo. Lakini kama ni kweli mtu huyo ndiye aliyetumika kulenga shabaha, basi kazi itakuwa imekwisha. Atakuwa ameua ndege wawili kwa jiwe moja.

"Mwingine ni Michael Sabuni. Huyu ana uwezo mkubwa wa sanaa za mapigano. Naye hukodiwa kwenye matukio ya kihalifu. Inasemekana na yeye alikuwepo kwenye kundi lililoua maharusi mwaka mmoja uliopita." Amour alizidi kushusha data.

Eddy alitambua kuwa huyo ndiye yule aliyepigana naye.

"Bosi pia kuna Tofiki Seif. Huyu ndiye dereva wao. Katika dodosa tu ni kwamba ana uwezo mkubwa wa kuendesha gari kwa kasi. Aliwahi kuwa bingwa wa mbio za magari miaka kadhaa nyuma. Kwa sasa majambazi wanamtumia kwenye shughuli zao. Wa mwisho wanaitwa Fadhili Kidaga, huku ni kama ndiye bosi wa msafara mzima ambao ulikuwa unakufuata." Amour alinyamaza na kumtazama bosi wake.

"Labda katika kuwabana wamesema ni sababu gani alikuwa wananifuata, na pia nani aliwatuma?" Eddy alimuuliza Amour.

"Bosi hapa inaonyesha kuwa lengo lao lilikuwa siyo kukuua wewe. Walitaka kumuua msichana uliyekuwa umeongozana naye, ila kama ikionekana kuna ulazima basi na wewe uuawe, lakini haswa ni huyo msichana."

"Wamewaambia ni nani yupo nyuma ya huu mpango?"

"Jim ndiye aliyewatuma. Na bosi tulivyofuatilia, tumegundua kuwa Jim ni ndugu wa George na Paul ambao tuliwakamata hivi karibuni kwa kosa la kula njama ya kumuua Fikiri kwa sumu."

"Basi kazi nzuri. Ila kuna nyongeza ya kazi hapa. Kwanza kabisa fanyeni kila njia, ili huyo jamaa Jim na ndugu yake Ben wakamatwe sawa?"

Amour aliitikia na kuagana na bosi wake. Eddy alirusha ngumi ya ushindi hewani. "Kazi inakaribia kwisha." alijisemea moyoni.

Kitendawili tayari kinaonekana kuwa kimeshaanza kuteguka. Alijua kuwa Jim na Ben ndiyo waliowatuma hawa jamaa kumuua Shani. Na hii ni baada ye ndugu zao kukamatwa. Na hata wao wenyewe wamejificha. Hawajulikani walipo kwani hata kwao hawaishi hapo kwa sasa.

Kingine, kwa namna ambayo hakutarajia tayari ameshapata mtu ambaye anahusika na mpango wa kumuua baba yake Shani, Patiyo mkewe Grace ambao walikuwa wametoka kufunga ndoa mashaa kadhaa tu yaliyopita.

Kwa jinsi sakata zima alivyolifuatilia, aligundua kuwa inawezekana Jim akawa amewakodi watu walewale ambao walimuua mdogo wake Patiyo bila yeye kujua ili wamuue Shani.

Anachojua kuwa Jim na ndugu zake wanataka kumuua Shani kwa sababu ya uchu wa mali, lakini kitu ambacho kimekuwa bado kinamuumiza kichwa je, Patiyo na shangazi yake Grace waliuawa kwa sababu gani?

Akainua simu ya mkononi. "Amour, nimesaahau kitu. Namhitaji Tamim Hussein kwenye eneo la tukio sawa?" Akakata simu baada ya kujibiwa.

Alijia kwa sababu Tamim anatajwa kuhusika na tukio hilo, basi ni yeye ndiye atakayekuwa anajua ni nani aliyewatuma kumuua Patiyo na mkewe na kwa sababu gani.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**




# SZOBOSZLAI AGOMBEWA LIGI KUU ENGLAND

**LONDON,** England

TIMU za Arsenal na Tottenham Hotspur zimeripotiwa zipo kwenye mbio moja za kuwania saini ya nyota wa Salzburg, Dominik Szoboszlai.

Szoboszlai mwenye umri wa miaka 20, amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kutoka Salzburg baada ya kung'ara kwenye klabu hiyo ya nchini Austria.

Huku pia klabu nyingine saba kubwa za Ulaya zikiwa pia zinamkodolea macho mchezaji huyo wa kimataifa wa Hungary.

Arsenal na Tottenham tayari zimeonesha kuwa ndio zinaongoza kwenye mbio za kuwania saini hiyo ya nyota huyo wa Salzburg, Szoboszlai, kwa mujibu wa Eurosport.

Lakini ripoti zaidi zinasema kwamba, RB Leipzig anaonekana kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kushinda kwenye mbio za kuwania saini ya nyota huyo.

Klabu za AC Milan na Atletico Madrid nazo zimeripotiwa kuwa na nia ya kuiwania saini ya mchezaji huyo.

# Zidane hana mpango wa kujiuzulu

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema kuwa "hatajiuzulu" hata baada ya kufungwa na Shakhtar Donetsk na kufanya matumaini ya kuingia kwenye raundi ya 16 bora ya Ligi ya mabingwa Ulaya kuwa magumu.

Real Madrid ambao ni wafalme wa ligi ya mabingwa Ulaya wakiwa wamelitwaa taji hilo mara 13, wanashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa kundi B, huku timu zote nne zikiwa zina nafasi ya kufuzu hatua raundi ya mwisho ya mechi wiki ijayo.

Real ni lazima iifunge Borussia Monchengladbach ili iweze kusonga mbele.

"Sitajiuzulu, siwezi," alisema Zidane baada ya kufungwa mabao 2-0 na Shakhtar akiwaambia waandishi wa habari.

"Nina nguvu zinazohitajika kubadilisha hali na nitafanya kila linalowezekana. Pamoja na wachezaji wangu.

Hiyo ilikuwa ni mara ya pili kwa Real kushindwa na Shakhtar msimu huu.

Shakhtar Donetsk haikuwa imeshinda mechi yoyote ile kati ya tatu za ligi ya mabingwa tangu ilipoicharaza Real Madrid mnamo mwezi Oktoba.





# *Klopp athibitisha kipa Allison nje wiki mbili*

**LIVERPOOL,** England

GOLIKIPA wa Liverpool, Alisson, atakuwa nje ya dimba kwa kipindi cha wiki mbili kwa mujibu wa Kocha Jurgen Klopp.

Alisson alikosa mchezo wa Ligi ya mabingwa Ulaya dhidi ya Ajax baada ya kupata jeraha la nyama za paja katika sare dhidi ya Brighton Jumamosi iliyopita,.

Na nyota huyo wa kimataifa wa Brazil hatakuwa sehemu ya mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya kwa Wolves Jumapili na dhidi ya FC Midtjylland kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Sio covid 19," alisema Klopp akiiambia BT Sport.

"Amepata majeraha na atakuwa nje ya dimba kwa wiki mbili, hivyo hatutakuwa nae kwa sasa."

"Sijawahi kusikia juu ya misuli ambao ni siku nne au tano tu kwa hivyo itakuwa siku 10 hadi 14, nadhani." aliongeza Klopp.

## Gattuso apewa mkataba mpya Napoli

**NAPLES,** Italia

GENNARO Gattuso amekubali mkataba mpya na miamba wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Napoli, kwa mujibu wa Mkurugenzi, Cristiano Giuntoli.

Gattuso mwenye umri wa miaka 42, kwa sasa mkataba wake na Napoli unamalizika mwishoni mwa msimu huu baada ya kuchukua mikoba ya Carlo Ancelotti, Desemba mwaka jana.

Tangu achukue mikoba hiyo, kocha huyo wa zamani wa Milan, Gattuso ameiongoza Napoli kushinda taji la Coppa Italia msimu wa 2019-20 likiwa taji la kwanza kwa klabu hiyo tangu mwaka 2014.

Giuntoli aliulizwa kuhusu majali ya Gattuso baada ya kutoka sare ya 1-1 na AZ kwenye Ligi ya Europa Alhamisi.

"Najua wanasheria wanabadilishana mikataba," alisema Giuntoli akiiambia Sky Sport Italia.

"Tumefikia makubaliano na mkataba ulikwisha andikwa wiki hii. Sidhani kama kutakuwa na tatizo lolote."

Napoli ipo nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu huu, ikipitwa pointi sita na vinara Milan baada ya mechi tisa.

Gattuso na Napoli kesho Jumamosi watakwenda kucheza na Crotone.





# PSG KUMUUZA MBAPPE WAKIMPATA MESSI

**PARIS,** Ufaransa

PARIS Saint-Germain italazimika kumuuza Kylian Mbappe kama watamsajili nyota wa Barcelona, Lionel Messi, kwa mujibu wa Diario AS.

Neymar alizungumzia kuhusu Messi baada ya kuripotiwa kwamba anataka kucheza tena na nyota huyo wa kimataifa wa Aregentina.

Neymar alifurahiaa mafanikio wakati akicheza na Messi kule Barcelona kabla ya kuondoka kwa ada iliyoweka rekodi mwaka 2017.

Na sasa Neymar anataka tena kucheza na Messi na kuna uwezekano mkubwa kwamba akatua pale Barcelona.

Messi amekuwa akihusishwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, PSG baada ya Neymar kueleza nia yake ya kutaka kuungana na mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or.

Na Messi akitua kwa miamba hao wa mji mkuu wa Ufaransa, Mbappe anaweza kuuzwa kwenda Real Madrid.

## *Messi anataka zaidi ya fedha Barcelona – Laporta*

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi anataka zaidi ya fedha pale Barcelona, huku mgombea wa urais Joan Laporta akisisitiza nyota huyo hana furaha kwa sababu ya timu kukosa mafanikio.

Majaliwa ya Messi yamebakia kuwa kitu muhimu kwa miamba hao wa LaLiga, Barca, baada ya kuomba kuondoka baada ya msimu mbaya wa 2019-20.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alikuwa akihusishwa na mpongo wa kujiunga na miamba wa Ligi Kuu ya England, Manchester City kabla ya kuamua kubakia nchini Hispania, ingawa sasa amekuwa akitajwa kuwaniwa na mabingwa wa Ligue 1, Paris Saint-Germain na Inter Milan.

Rais wa muda wa Barca, Carlos Tusquets, amesema klabu hiyo ilitakiwa kumuuza Messi katika dirisha lililopita kutokana na matatizo ya kifedha baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

Lakini Laporta, ambaye anawania urais katika uchaguzi unaofanyika Januari 24 mwakani baada ya kujiuzulu kwa Josep Maria Bartomeu oktoba, amezungumzia kuhusu Messi.

"Leo anaitaka Barcelona," alisema raia huyo wa zamani Laporta – ambaye alikuwa kwenye nafasi hiyo kutoka mwaka 2003 hadi mwaka 2010 akiiambia redio Marca and COPE.

"Kitu ninachotaka kurudisha ni furaha. Ni swali kuhusu fedha, unatakiwa kutengeneza timu ya ushindi.

"Leo amedanganywa na hilo ni pigo kubwa. Yeye ni mshindi na hawezi kusima ma na kuona timu nyingine zikishinda Ligi ya mabingwa Ulaya.

"Mara ya mwisho nimezungumza nae Oktoba. Nina furtaha kubwa kwake kwa kile alichokifanyia Barcelona. Tangu akiwa na umri wa miaka 16 ni mtu wa aina yake."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# WOODWARD: MAN U IPO PAMOJA NA SOLSKJAER

●●● Kile kinachotokea dimbani kwa uhakika kabisa tuko pamoja naye...

**MANCHESTER,** England

MAKAMU mwenyekiti Mtendaji wa Manchester United, Ed Woodward kwa mara nyingine amemuunga mkono Ole Gunnar Solskjaer na kusema mipango ya muda mrefu wa klabu hiyo ipo na raia huyo wa Norway.

Solskjaer anakaribia miaka miwili tangu ateuliwe kuwa kocha wa United, awali akipewa majukumu kwa muda kabla ya kupewa mkataba wa kudumu na amekuwa akishutumiwa kwa muda mrefu.

Alianza kuwa kwenye presha baada ya kufungwa na Arsenal na Istanbul Basaksehir mwezi uliopita, lakini Woodward amesema klabu ipo pamoja na mshambuliaji wake huyo wa zamani.

"Kile kinachotokea dimbani kwa uhakika kabisa tuko pamoja naye.

**"Ingawa mambo yamebadilika kwa kucheza bila mashabiki uwanjani, tumeona mambo mengi na nina uhakika kwamba mambo yatabadilika.**

"Tulicheza mechi 14 bila kufungwa na tukamaliza nafasi ya tatu msimu uliopita na tukapata ushindi mkubwa dhidi ya PSG na RB Leipzig kwenye mechi ya marudiano kwneye Ligi ya mabingwa msimu huu.

"Bilashaka tunatambua kwamba hii ilikuwa ni kazi kubwa na mafanikio makubwa kwa timu na sasa tunahitaji kushinda mataji.

"Lakini tumeona ishara uwanjani na kwenye mazoezi na tuna imani kubwa kwamba tuna nafasi ya kufanya vizuri na Ole kuendelea kuwa kocha wetu.

"Tuko pamoja na Solskjaer na tunamuunga mkono kwa asilimia 100, tutampa ushikirikiano wote wakati wa dirisha la usajili la Januari."

## ZISIKUPITE

### AGOMBEWA ARSENAL, CHELSEA

ARSENAL na Liverpool zipo kwenye mbio moja kumwania kiungo wa kati wa Brighton na Mali, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 24. ***(Talksport)***

### RUDIGER, TOMORI KUONDOKA

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger, 27, na mlinzi wa England, Fikayo Tomori, 22, wanaweza kuondoka kwenye klabu hizo wakati wa dirisha la Januari.

### MILIK AWANIWA

KLABU za Tottenham Hotspur, Everton na Atletico Madrid zinamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa Napoli, Arkadiusz Milik mwenye umri wa miaka 26 raia wa Poland. ***(AS)***

### IBSEN KUSAJILIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham imeripotiwa inataka kumsajili mlinzi wa timu ya taifa ya Denmark chini ya umri wa miaka 21, Frederik Alves Ibsen mwenye miaka 20, kutoka Silkeborg kwa pauni milioni 1.2 wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Sky Sports)***

### DEMBELE NA MKATABA MPYA

KLABU ya Barcelona imeanza mazungumzo na mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele, 23, kuhusu mkataba mpya, huku Manchester United nao wakiendelea kumsaka mchezaji huyo. ***(ESPN)***

### SOLSKJAER AFUKUZWE

MANCHESTER United wanapaswa kumfuta kazi kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer na nafasi yake ichukuliwe na ama Mauricio Pochettino, Antonio Cone au Diego Simeone, amesema mmiliki wa zamani wa Crystal Palace, Simon Jordan. ***(Talksport)***

### ROONEY NA UKOCHA

WAYNE Rooney amesema bado anapendelea kuwa kocha wa kudumu katika klabu ya Derby County, licha ya mchezaji mwenzake wa zamani wa England, John Terry kuhusishwa na kazi yake. ***(Goal)***

### ZAHA ASAJILIWE ARSENAL

ARSENAL wanatakiwa kumsajili mshambuliaji wa kati wa Crystal Palace raia wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, mwenye umri wa miaka 28, kwa mujibu wa David Seaman, ambaye alishinda mataji matatu ya ligi na vikombe vinne vya FA akiwa na washikabunduki hao. ***(Evening Standard)***

### MOURINHO NA UKOCHA

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho mwenye umri wa miaka 57, anaamini kuwa bado ana miaka 15 hadi 20 iliyobaki katika kazi yake ya kufundisha, ikimaanisha kuwa anataka kuendelea kuwa kocha hadi akiwa na umri wa miaka 70 na zaidi. ***(Sport)***

### TORREIRA ANA NAFASI ARSENAL

KIUNGO wa Arsenal, Lucas Torreira, mwenye umri wa miaka 24, bado ana nafasi pale Emirates licha ya sasa kupelekwa kwa mkopo kule Atletico Madrid, amesema Gilberto Silva. ***(Sun)***




Wanariadha wa timu ya Mkoa wa Dar es Salaam wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kujiandaa na mashindano mbalimbali yanayotarajiwa kufanyika hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA YAKANUSHA KUMRUDISHA OKWI

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema kuwa mpaka sasa haina mpango wa kumrejesha mchezaji wao maarufu wa zamani, Emmanuel Okwi, huku ikidai kuwa ina mpango wa kusajili wachezaji wawili kuongezea nguvu kikosi.

**Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano Klabu ya Simba, Haji Manara, amesema kuwa mpaka sas hakuna mpango wowote wa kumrejesha Mganda huyo ambaye ni kipenzi cha wanachama na mashabiki wa Simba.**

"Binafsi kama mimi ukiniambia ningependa arudi, ni rafiki yangu sana, lakini mpaka sasa kama klabu bado haijawa na mpango huo, labda hapo hapo baadaye siku za usoni," alisema Manara.



Manara amemaliza uvumi wa baadhi ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kudai kuwa Simba iko mbioni kumrejesha tena kwa mara ya tatu mchezaji huyo ambaye amekuwa akiipa heshima klabu ya Simba kila anaporejea, kutokana na hali yake ya kujituma na upambanaji, akiwa anaibeba timu ya Simba kwenye mechi kubwa.

Kwa sasa mchezaji huyo anaichezea klabu ya Ligi Kuu nchini Misri El Ittihad.

Okwi alisajiliwa na Simba mwaka 2009, akitokea SC Villa ya Uganda na akauzwa 2013 kwenye klabu ya Etoile du Sahel ya Tunisia, lakini mwaka mmoja baadaye akarejea SC Villa kabla ya kutimkia Yanga ambako alicheza kwa muda mfupi, akarejea Simba ambapo alicheza hadi 2015, akaelekea Sonderjyske ya nchini Denmark, lakini alirejea tena Simba 2017 hadi 2019 ambapo alielekea nchini Misri.

Wakati huo huo, klabu ya Simba imesema kuwa iko mbioni kusajili wachezaji wawili kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mwina Kaduguda, alisema kuwa baada ya kumsajili kiungo mkabaji Thadeo Lwanga kutoka nchini Uganda, ina mpango wa kusajili mshambuliaji mmoja na beki mmoja.

# SportPesa watambulisha Kasino kwenye simu janja

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo na burudani SportPesa, imeendelea kuonyesha ubunifu kwa wateja wake kwa kutambulisha programu maalum ya mchezo wa Kasino kwa watumiaji wa simu janja (android).

Hii ikiwa ni muendelezo wa awamu nyingine baada ya kutambulisha huduma hii kwa watumiaji kupitia tovuti yao ya www.sportpesa.co.tz

Akizungumza mara baada ya uzinduzi huo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa Tanzania ,Tarimba Abbas alisema: "Ni furaha kubwa kwetu kuzindua rasmi huduma ya mchezo wa kasino kwa watumiaji wa simu za android kwa kuweza kupakua aplikesheni yetu ya Kasino kupitia link maalum kupitia simu zao za mkononi.

"Ndani ya SportPesa Kasino kuna michezo zaidi ya mia moja huku ikimpa nafasi mchezaji kuweka dau kuanzia Sh. 20 kulingana na mchezo.

"Hii ni nafasi njema kwa mteja wetu, kwani tumempa uwezo wa kuhamisha fedha kutoka kwenye pochi ya kubet michezo mbalimbali na kuweka kwenye pochi ya Kasino bila gharama yoyote," alisema.

Alisema lengo kuu pamoja na kuburudisha na kumpa fursa mteja kuzidi kufurahia huduma zao huku wakiendelea kutoa huduma saa 24 kwa ubunifu wa hali ya juu.

"Hadi sasa SportPesa imeongeza masoko mbalimbali kupitia tovuti yao ya www.sportpesa.co.tz kama Jenga bet, Jackpot, Michezo halisi huku vyote hivi vikipatikana wa watumiaji wa mitandao yote ya simu.

## Salamba kuiokoa Rabita

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Namungo FC, Adam Salamba, atakosa mechi ya marudiano dhidi Al Rabita FC ya Sudan Kusini kwenye kombe la Shirikisho Barani Afrika, utakaopigwa kesho Jumapili, uwanja wa Azam Complex.

Salamba aliumia katika mchezo wa kwanza wa kombe hilo uliopigwa katika uwanja huo huku Namungo iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 katika mchezo huo Al Rabita wakiwa ugenini.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Namungo, Hemed Morocco, alisema watamkosa Salama ambaye amepata majeraha katika paja ila wachezaji walibakia wako fiti.

Alisema mbali na kumkosa nyota huyo ana imani ya kufanya vizuri katika mechi hiyo ya marudiano kuhakikisha wanavuka hatua ya pili ya kombe hilo.

## Mambeza kideoni

**Na Sabato Kasika**

NYOTA wa muziki wa kizazi kipya, mwanadada Pamela Daffa (Pam D), ambaye sasa anatamba na wimbo mpya wa 'Mambeza', amesema anajiandaa kutambulisha video wiki ijayo.

Akizungumza na gazeti hili, msanii huyo anasema alipanga kutambulisha video hiyo mwezi uliopita, lakini akashindwa kutokana na matatizo ya mtandao, na hivyo kulazimika kusubiri hadi hali iwe nzuri.

Msanii huyo amesema, katika wimbo huo unaotamba sasa, amemshirikisha mwimbaji mkongwe wa muziki wa mwambao Patricia Hilary. aliyewahi kutamba na nyimbo mbalimbali ukiwamo wa 'Ewe Njiwa Peleka Salaam'.

Aidha, amesema tangu aanze muziki wa kizazi kipya amekuwa akiwashirikisha wasanii mbalimbali wa muziki wa kizazi kipya, dansi na hata taarab, kwa lengo la kupata ladha tofauti katika nyimbo zake.

# Michezo

Jumamosi Desemba 5, 2020

Nipashe




'Man United ipo pamoja na Solskjaer' UKURASA 22



Wachezaji wa timu ya LSL, wakishangilia ubingwa na kombe lao baada ya kuifunga timu ya Ballymun mabao 4-2 na kuibuka mabingwa katika mashindano ya ligi ya soka ya walemavu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA 'TIK TAKA' KWA MKAPA LEO

## ●●● Ni katika mechi yao dhidi ya Plateau ya Nigeria, Sven atabiri mchezo mgumu...

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, leo wanatarajia kujitupa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza mechi ya mkondo ya pili dhidi ya Plateau United ya Nigeria, kuwania kuingia raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

**Mechi hiyo inatarajiwa kucheza saa 11:00 jioni, huku mabingwa hao wa Tanzania wakiwa na kumbukumbu ya kushinda bao 1-0 ugenini kwenye Uwanja wa New Jos, Abuja nchini Nigeria Jumapili iliyopita.**

Katika mechi hiyo, Simba inahitaji ushindi au sare yoyote ile ili asonge mbele na kukutana na mshindi kati ya FC Platinum ya Zimbabwe na Costa do Sol ya Msumbuji kwenye mechi ya raundi ya kwanza.

Hata kama itapoteza, Simba inatakiwa ipoteze kwa mabao 2-1 tu, ambapo itasonga mbele kutokana na bao la ugenini, zaidi ya hapo itakuwa imetolewa kwenye michuano hiyo, lakini kama itafungwa bao 1-0 timu hizo zitalazimika kupigiana mikwaju ya penalti tano tano.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema kuwa mechi itakuwa ngumu kutokana na wapinzani wao kuwa ni wazuri, lakini amewaandaa wachezaji wake kupambana kwenye mechi ya nyumbani ikiwa mbele ya mashabiki wa klabu hiyo kama ilivyofanya kwenye mechi iliyopita.

"Tuna dakika zingine 90, Plateau United ni timu nzuri na ina wachezaji wazuri wanaocheza kwa kasi na kutumia nguvu, lakini tumejiandaa na mechi hii ili tusonge mbele," alisema kocha huyo.

Kocha huyo pia alieleza kufurahishwa na kiwango cha uzuiaji kilichoonyeshwa na wachezaji wake mechi iliyopita na kuonyesha kuwa hali hiyo ni nzuri kwa mechi ya leo na za baadaye kwani, tayari vijana wake wameimarika kwenye hilo.

Simba itabidi iwachunge wachezaji hatari wa timu hiyo kama Sunday Adetunji, Gabriel Wassa, Saed Jibril na Issa Ndala ambao waliwasumbua sana mabeki wa timu hiyo, wakiongozwa na kipa Aishi Manula.

Kwenye mechi iliyopita, Simba ilipata bao pekee dakika ya 53 likifungwa na Cleotus Chama na kuifanya timu hiyo kuonekana kama imetangulia mguu mmoja kutinga raundi ya kwanza.

Simba ina kumbukumbu ya kutolewa kwenye raundi ya awali msimu uliopita dhidi ya UD Songo, huku mwaka 2018 ikifika hatua ya robo fainali na kutolewa na TP Mazembe kwa mabao jumla ya mabao 4-1.

# Kaze azungumzia ubingwa Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze (pichani chini), amesema suala la ubingwa kwao lipo chini ya wachezaji kuendelea kujituma na kupambana katika kutafuta matokeo kwenye michezo yao yote ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Kaze alisema anaendelea kusisitiza wachezaji wake kutimiza malengo yao ili kuchukuwa ubingwa na kutotoka katika nafasi hiyo ya kwanza waliyopo.

Alisema baada ya kumalizika kwa mechi yao dhidi ya JKT Tanzania alikaa na kuzungumza na wachezaji wake, na kuwataka kuendelea na kasi hiyo waliyoianza katika mzunguko wa kwanza kabla ya kwenda wa pili.

"Tunaendelea kuimarisha kikosi changu, wachezaji wanapambana kuhakikisha timu inabaki kileleni, malengo yetu ni kuendelea kuongoza hadi mwisho wa ligi,"



"Hakuna mbinu zaidi ya kufika huku ni wachezaji kujituma na kujitolea wakati wa kutafuta ushindi katika mechi zilizopo mbele yetu," alisema Kaze.

Alisema kwa sasa anaendelea kuwapa mbinu washambuliaji wao kuwa makini na watulivu hasa wanapopata nafasi uwanjani katika mechi zao za ligi hiyo.

"Suala la ubingwa ni juhudi na kupambana kwa wachezaji kuhakikisha tunachukulia umuhimu kila mechi kutafuta ushindi kwa sababu ligi ni ngumu," alisema Kaze.

Yanga ipo nafasi ya kwanza ikiwa na pointi 31 inafuatiwa na Azam FC iliyo nafasi ya pili na pointi 26 zote zimecheza mechi 13 huku Simba ikiwa nafasi ya tatu na pointi 23 baada ya kucheza mechi 11.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >